Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Musa akawaambia kaumu yake: Ombeni msaada kwa Allah na subirini. Hakika ardhi ni ya Allah, Atairithisha Amtakaye katika watumishi Wake; na mwisho (mwema) ni kwa wamchao. (Al-A'raaf 7:129)

JUZU 82 No. 229 | JAM.II-RAJAB.1443 AH | FEBRUARI 2022 | TABLIGH 1401 HS | BEI TSH. 500/=

Bishara Tukufu kuhusu Mwana Aliyeahidiwa[ra]



Kila mwaka, mwezi wa pili unapoingia unatukumbushia bishara tukufu sana ya Hadhrat Masihe Maud[as] kumhusu Mwana wa ahadi anayejulikana zaidi kwa jina la Musleh Maud[ra] aliyekuwa Khalifa wa pili wa Sayyidna Ahmad[as]. Kwa hakika bishara hii ilitolewa na Kipenzi hasa wa Allah na kiumbe bora mno wa Allah[swt] ambaye ni Mtume wetu Muhammad, amani, baraka na rehema zisizohesabika ziwe juu yake daima dawamu katika ulimwengu wote.

Bwana wetu mpendwa, Mtume Mtukufu[saw] alisema *kabla karne kumi na nne akitufafanulia ujaji wa pili wa Msihi na Imam Mahdi katika umma wa Waislamu kwamba: Masihi aliyeahidiwa ataoa na atajaliwa kizazi adhimu.* (Mishkat bab nuzule Issa)

Sayyidna Ahmad[as] alisema akieleza maneno haya ya Mtume Mtukufu saw kwamba, Allah Atamjalia na Mwana mwema atakayekuwa mfano wa babake na kuwa mtiifu wake kwa kila jambo kisha atakuwa miongoni mwa watu watukufu wa Allah[swt].

Tunaposoma historia yetu tunapata kujua kuwa; Sayyidna Ahmad[as] alitangaza tangazo maalum kwa ufunuo wa Allah na kuwaita watu kuja Qadian kwa ajili ya kushuhudia ishara hai juu ya Kudra ya Allah mnamo 1885. Na Mabaniani wa Qadian walimwomba Sayyidna Ahmad[as] kwa barua yao kwamba sisi ni Jirani zako na wakazi wa Qadian hivyo tunahaki zaidi ya kuona ishara ya aina hivyo ili tuelewe kuwa Allah husikia maombi yako na hukupa habari za ghaibu, zisizoonekana kidhahiri.

Sayyidna Ahmad[as] aliwajibu mabaniani hawa akikubali ombi lao kwamba kama mtayafuata yale masharti mliyoyakiri katika barua yenu basi lazima Allah Atadhihirisha ishara ndani ya muda wa mwaka mmoja, itakayokuwa nje ya uwezo wa binadamu. (Majmuae Ishtiharat J.1.UK.91)

Sayyidna Ahmad[as] aliambiwa na Allah ili aende mjini Hushyarpur na kupata wahyi mnamo January 1886 kwamba *utasaidiwa na kuondolewa shida mjini Hoshyarpur. (Teri ukda kushai Hoshyar pur me hogi)*

Seyydna Ahmad[as] alifunga safari ya kuelekea Hoshyarpur kutokana na ufunuo huu mnamo 22 January 1886 pamoja na marafiki zake watatu na kukaa huku nyumbani kwa Sheikh Mehr Ally Sahib kwa siku 40. Huzur alichagua ghorofa ya juu ya nyumba hiyo na kufanya maombi mfululizo wala hakuonana na yeyote mwingine ndani ya siku hizo 40 hata sala ya Ijumaa alikuwa anasali na marafiki hao

Endelea uk. 3

Uchawi - Imani za kishirikina

Afafanua Sheikh Hussein Ng'amilo wa Zanzibar









Kwa mujibu wa Qur'an Tukufu kuna aina mbili za sihr/ mazingaombwe;

Uchawi huu ni wa kufikirika [imagination] na wa dhana tu ambao umetajwa katika Qur'an kwenye matukio ya Hadhrat Musa[as] na watu wa Firauni walio kusanywa pamoja siku waliyokuwa wameahidiana.

Wa pili ni yale **mazingaombwe** ya makundi ambayo yanataka kudanganya watu kwa njama na kushawishi pamoja na kueneza uvumi katika Jamii kwa ajili ya kushusha hadhi na heshima ya serikali na kuiasi. Uchawi huu pia umeelezwa kwenye sura Al Falaq.

Maana ya neno sihir [uchawi]

SIHIR; neno hili kwa Kiswahili lina maana hizi mbili; moja kiini macho, na mbili ni uchawi. Katika lugha ya kiarabu SAAHIR lina maana nyingi kama linavyoelezwa hapa kuwa neno hilo sio kila mara liwe na tafsiri ya mchawi pia lina maana sita zingine zinazopatikana kwenye kamusi ya Akrab na Lane.

1. Mlozi.
2. Mtu anayeliwaza na kutumbuiza.
3. Mtu anayejua, stadi mwenye akili.
4. Mtu mwenye uwezo wa kukifanya kitu kionekane namna nyingine kuliko hasa kilivyo.
5. Mdanganyaji
6. Mlaghai

Katika kamusi ya lisaanul Arab iliyo andikwa na Al-Azhar ame toa maana ya neno Assihr "*kulibadilisha jambo mbali na uhakika wake, nako ni kuwadhihirishia watu jambo lisilo la kweli wakaliona kuwa ni la kweli.*"

Sahaba wa Mtume, Hadhrat Ibn Abbas[ra] anasema kuwa ***"uchawi ni kudhihirisha batili katika sura ya haki"***

Hapa tunaona sahaba wa Mtume ambaye aliombewa na Mtume[saw] ALLAHUMMA FAKKI HUL QUR'AN [Yaani Eee Allah

Endelea uk. 5

Utalii wa ndani uk. 2

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

UTALII WA NDANI

Usipotenga muda kidogo wa kukaa na kutafakari, basi yote unayoyaona unaona yalitakiwa yawe hivyo na wala hakuna la ajabu. Hilo ni kosa kubwa sana. Ni maajabu yanayotuzunguka yanayokulazimisha kuanguka chini kusujudu na kutoa shukurani kubwa kwa Allah.

Kaa chini utafakari juu ya nchi nzuri iitwayo Tanzania tuliyopewa na Allah. Ardhi nzuri na yenye rutuba. Misitu minene inayoongeza uzuri wa mandhari. Mito inayotiririka katika safari ile isiyokwisha. Maziwa makubwa yanayotusaidia katika usafiri. Bahari ambayo sasa imetukumbusha uchumi wa bluu. Mlima mrefu kuliko yote katika bara la Afrika. Utawezaje kuzihesabu neema zote alizokupa Allah? Huwezi.

Kwa hili tunao wajibu wa kumshukuru Allah kwa neema hizi alizotujaalia. Hakuzisitisha, je tunazitambua neema hizi? Tunazienzi? Tunazitunza? Tuna ghari nazo? Tunajali?

Watalii kutoka nje ya nchi wanamiminika nchini mwetu kuja kujionea maajabu tuliyopewa na Allah.

Ni vyema kukumbuka kuwa si watalii wote ni matajiri. La hasha. Baadhi ni wafanyakazi wa kawaida ambao wamedunduliza ili kuja Tanzania kujionea neema hii kubwa tuliyopewa.

Inasikitisha mtu anafunga safari masafa hayo marefu kuja kujifunza, kuja kushangilia maumbile na sisi wenye nchi wala mshipa hautugongi. Ni vizuri tukabadilika.

Mapenzi kwa nchi yetu inabidi yaongezeke. Hii ni nchi nzuri na yenye kila sifa. Tufanye bidii ya makusudi kuifahamu. Tufahamu historia yake, utajiri tulio nao. Na kuifahamu tutoe kipaumbele kwa utalii wa ndani. Faida zake ni nyingi. Kuifahamu nchi yako na kuongeza maombi ya shukurani kwa neema hiyo. Unaongeza pato la taifa. Na ukweli kila mmoja wetu ana mchango wa kulitumikia taifa hili.

Jitihada za Rais wa nchi, Samia Suluhu Hassan za kuvuta watalii zinatakiwa zianze nyumbani.

Tupate mwamko mpya wa kulitangaza taifa letu. Watu wa mataifa mbalimbali wanapokutana wanabadilishana mawazo na heshima inajengeka. Waswahili husema asiyekujua hakuthamini. Safari hizo za watalii ni daraja la kuwavusha watu wa mataifa mbalimbali kukutana na kujifunza.

Watanzania tukumbuke kuwa vivutio vyote tulivyonavyo ni amana tuliyopewa na Allah na tuitunze amana kwa ajili ya binadamu. Ni heshima kuwa sisi tumepewa jukumu la kuwa walinzi wa hazina hizi ambazo hazipatikani mahali popote pale duniani. Hilo linatuongezea wajibu.

Wajibu wa kulinda amani na mshikamano wetu ili wanaokuja kututembelea wakute usalama na amani. Taifa letu lina sifa ya ukarimu kwa wageni, huu ni utamaduni mzuri tunaotakiwa kuuendeleza. Kutunza mazingira yetu ndio roho ya mafanikio yetu. Kuharibu mazingira kutakuwa na athari mbaya, hivyo tuyatunze kwa kutokata miti au kuingia vyanzo vya miti. Kazi hii ni kubwa na nzito. Na haiwezi kuwa kazi ya kundi fulani au shirika fulani, hili ni jukumu la kila mzalendo wa nchi hii.

Allah Atujaalie kutimiza wajibu wetu, Amin.



QUR'AN TUKUFU

Sura Aal-Imran : 55

إِذْ قَالَ اللَّهُ يَا عِيسَىٰ إِنِّي مُتَوَفِّيكَ وَرَافِعُكَ إِلَيَّ وَمُطَهِّرُكَ مِنَ الَّذِينَ كَفَرُوا وَجَاعِلُ الَّذِينَ اتَّبَعُوكَ فَوْقَ الَّذِينَ كَفَرُوا إِلَىٰ يَوْمِ الْقِيَامَةِ ۖ ثُمَّ إِلَيَّ مَرْجِعُكُمْ فَأَحْكُمُ بَيْنَكُمْ فِيمَا كُنتُمْ فِيهِ تَخْتَلِفُونَ

(Kumbukeni) Allah aliposema: Ewe Isa! kwa yakini Mimi Ndiye Mwenye kukufisha, na kukuinua kwangu, na Nitakutakasa na (masingizio ya) wale waliokufuru, na nitawaweka wale waliokufuata juu ya wale waliokufuru, mpaka Siku ya Kiyama. Kisha marudieo yenu ni Kwangu, ndipo Nitawahukumuni katika yale mliyokuwa mkikhitalifiana.

NUKUU YA HADITHI

عن عبد الله بن عمرو قا ل قا ل رسول الله صلى الله عليه وسلم ينزل عيسى بن مريم إلى الأرض فيتزوج ويولد له ويمكث خمسا وأربعين سنة ثم يموت فيدفن معي في قبري فأقوم أنا وعيسى بن مريم في قبر واحد بين أبي بكر وعمر

Imesimuliwa na hazrat Abdullah bin Amri r.a. ya kwamba Mtume saw alisema: atashuka Issa bin Maryam kwenye ardhi basi atoa na atajaliwa kizazi (cha kutumikia dini). Na atakaa ardhini miaka arobaini na mitano(yaani baada ya kutangaza madai ya kuwa ametumwa) kisha atafariki na atazikwa pamoja nami katika kaburi langu. Hivyo mimi na Issa bin Maryam tutainuka kutoka kaburi moja baina ya Abu Bakr na Umar. (Mishkat Bab nuzule Issa).

ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA[as]

Mwana Aliyeahidiwa

Seyyedna Ahmad a.s. anasema:(tafsiri ya kiarabu): Mtume saw alitoa bishara kwamba: kwa Yakini, Masihi Aliyeahidiwa ataoa na kujaliwa na kizazi. Kwa kweli imedokezwa ndani ya (maneno) hayo kwamba, kwa Yakini Allah mtukufu Atamjalia Mtoto mwema ambaye atakuwa mfano wa baba yake wala hatakuwa dhidi yake kisha atakuwa miongoni mwa watu watukufu wa Mwenyezi Mungu. (Aainae Kamalate Islam,Rohani Khazain J.5.UK.578)

Kisha anasema katika kitabu chake "Tuhfae Baghdad":(tafsiri): kuna dokezo kwenye (bishara) hiyo kuwa: huyu (Masihi Aliyeahidiwa) atazaliwa mwana mwema ambaye atakuwa mithili yake kutokana na sifa na ubora wake. (Tuhfae Baghdad,Rohani Khazain j.7.uk.209)

Hakika kwa ajili ya Mahdi wetu kuna ishara mbili ambazo hazijatokea (kwa kuhakikisha ukweli wa mdai ye yote) tangu ziumbwe mbingu na ardhi, nazo ni hizi: Mwezi utapatwa siku ya kwanza (miongoni mwa tarehe za kupatwa kwake) katika Ramadhan, na Jua litapatwa siku ya katikati (baina ya tarehe za kupatwa kwake) katika mwezi huo huo (wa Ramadhan). Wala hazijatokea ishara hizo (kwa ajili ya mdai ye yote) tangu kuumbwa kwa mbingu na ardhi.

[Dar Kutni] (Sunan Dar Kutni, bab sifatu Salatil khusufi wal kusufi, j.1. uk.188)

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Ahmad Abdul Nasibu.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Maisha ya Mtume Muhammad saw

Yalivyosimuliwa na Hadhrat Mirza Bashir ud Din Mahmud Ahmad r.a. Khalifatul Masih wa pili wa Masihi Aliyeahidiwa[as]

Inaendelea Kutoka toleo lililopita

Kufuatwa na Suraka na bishara ya Mtume[saw] Kuhusiana naye

Watu wa Makka waliposhindwa katika juhudi zao za kumtafuta, basi wakatangaza kwamba yeyote atakayewarejesha Muhammad s.a.w. au Abu Bakar r.a. wawe hai au mauti, huyo atapewa zawadi ya ngamia mia moja. Na habari ya tangazo hili likapelekwa kwa makabila yaliyokuwa pembezoni mwa Makka. Hivyo kiongozi fulani wa kibedui, aliyeitwa Suraka bin Maalik, akafunga safari ya kuwafuatilia kwa tamaa ya kuipata zawadi hiyo. Aliendelea kutafuta hadi akawakuta katika njia ielekeayo Madina. Alipowaona ngamia wawili na wasafiri wake, basi akafahamu kwamba huyo ni Muhammad s.a.w. tu na wenzake. Hivyo akamkimbiza kwa kasi farasi wake kuwafuata. Lakini njiani yule farasi akajikwaa kwa nguvu na Suraka akaanguka chini.

Huyu Suraka baadae alisilimu naye mwenyewe analieleza tukio lake kwa namna hii kwamba: Nilipoanguka na farasi, basi sawa na desturi za waarabu, nikatoa mishale yangu ya kupigia ramli na majibu ya ramli yakawa mabaya. Lakini kutokana na tamaa ya zawadi ile, nikampanda tena farasi na kuwafuata. Mtume s.a.w. alikuwa akiendesha ngamia wake kwa utulivu. Hakugeuka kunitazama. Lakini Hadhrat Abu Bakar r.a. mara kwa mara alikuwa akigeuka nyuma kunitazama (kwa hofu hii kwamba Mtume s.a.w. asipatwe na dhara yoyote).

Nilipowakaribia kwa mara ya pili, farasi wangu akajikwaa tena nami nikaanguka kwa kishindo. Hapa pia nikapiga tena ramli na matokeo yakawa mabaya. Niliona kwamba miguu ya farasi ilikuwa imezama mchangani kiasi ya kwamba ilikuwa vigumu kuichomoa. ndipo nikafahamu kwamba watu hawa wamo ndani ya ulinzi wa Mwenyezi Mungu. Nikawaita kwa sauti nikiwaambia simameni mnisikilize. Watu hao walponijia, nikawaambia kwamba mimi nilikuja huku kwa dhamira hii lakini sasa nimebadili dhamira yangu nami narejea, kwani nimekuwa na yakini kwamba Mungu yu pamoja na nyie watu.

Mtume s.a.w. akasema: Vizuri sana, nenda, lakini usimwambie yeyote kuhusiana nasi. Wakati huo likanijia wazo moyoni kwamba kwa kuwa mtu huyu anonekana kuwa ni mkweli, hivyo ni lazima siku moja atafanikiwa. Nilipojiwa na wazo hili, nikamuomba kwamba niandikie ujumbe wa amani kwa ajili ya wakati ule utakapopata ushindi. Yeye (Mtume s.a.w.) akamuagiza mtumishi wa Hadhrat Abubakar aliyeitwa Aamir bin Fahiira kwamba aandikiwe ujumbe wa amani. Hivyo akauandika ujumbe wa amani. Suraka alipokuwa anaondoka, basi wakati huo huo Mwenyezi Mungu Akamfunulia (Mtume s.a.w.) habari za ghaibu zijazo za Suraka na kuhusiana naye akamwambia: "Suraka! Utakuwa na hali gani wakati ule bangili za Kisra zitakapokuwa mkononi mwako." Suraka akauliza kwa mastaajabu: "Kisra bin Hurmuz aliye mfalme wa Iran?" Akamjibu "Naam."

Bishara yake hii ikatimia neno kwa neno baada ya miaka kumi na sita kumi na saba hivi. Suraka akaja Madina baada ya kusilimu. Baada ya kifo cha Mtume s.a.w., kwanza Hadhrat Abu Bakar r.a. akawa Khalifa, kisha Hadhrat Umar r.a. Baada ya kuiona shani iliyokuwa ikiongezeka ya Islam, Wairani wakaanza kuwashambulia Waislamu na badala ya kuiangamiza Islam, wenyewe wakaangamizwa walipopambana na Islam. Markaz ya Kisra ikaangamizwa kwa sauti za nyayo za farasi za waislamu na hazina ya Iran ikamilikiwa na Waislamu. Kati ya ile mali ya ufalme ule iliyotekwa na jeshi la Waislamu, mlikuwemo pia na bangili zile ambazo, sawa na desturi ya Iran, Kisra alikuwa akizivaa wakati wa kuketi kwenye kiti cha enzi.

Baada ya Suraka kusilimu, alikuwa akiwasimulia Waislamu kwa fahari sana tukio hili lililomtokea wakati wa Hijra ya Mtume s.a.w. na Waislamu walikuwa wanalifahamu jambo hili kwamba Mtume s.a.w. alimwambia "Suraka utakuwaje wakati ule bangili za Kisra zitakapokuwa mikononi mwako."

Mali za mateka zilipowekwa mbele ya Hadhrat Umar r.a. na kuziona humo Bangili za Kisra, basi ramani nzima ikachoreka mbele yake, wakati ule wa unyonge na udhaifu ambapo Mtume wa Mwenyezi Mungu alilazimika kuiacha nchi yake na kuja Madina. Yule Suraka na watu wengine waliokuwa wakimfukuza (Mtume s.a.w) kwa farasi ili wamfikishe kwa watu wa Makka akiwa hai au mfu ili wapate ngamia mia moja.

Kwa wakati huo kumwambia Suraka kwamba; Suraka utakuwa na hali gani wakati ule bangili za Kisra zitakapokuwa mikononi mwako, ilikuwa ni bishara kubwa ya aina gani na ilikuwa ni ghaibu iliyoonekana kwa uwazi kiasi gani. Hadhrat Umar r.a. akaziona bangili za Kisra mbele yake, basi uwezo wa Mwenyezi Mungu ukadhihirika tena mbele ya macho yake. Akasema "Mwiteni Suraka!" Suraka akaitwa basi Hadhrat Umar r.a. akamuagiza kwamba azivae mikononi mwake bangili za Kisra. Suraka akasema: Ewe Khalifa wa Mtume wa Mwenyezi Mungu! imekatazwa kwa waislamu kuvaa dhahabu! Hadhrat Umar r.a. akasema "Naam imekatazwa, lakini sio katika mazingira kama haya.

Allah Alimuonyesha Mtume Muhammad s.a.w. bangili za Kisra zikiwa mikononi mwako. Aidha uzivae bangili hizi au nikuadhibu. Lawama iliyotolewa na Suraka ilikuwa inatokana tu na masuala ya kisheria, waila hata yeye mwenyewe alikuwa akitamani kuiona bishara ya Mtume s.a.w. ikitimia. Suraka akaivaa mkononi bangili ile na Waislamu wakaona kwa macho yao bishara hii adhimu ikitimia.

Bishara kumhusu Mwana Aliyeahidiwa[ra]

Kutoka uk. 1

watatu. Huzur[as] alikesha usiku na mchana katika maombi na ibada kwa siku hizo zote na kutokusema na yeyote.

Allah Alimfungulia Hadhrat Ahmad[as] milango ya baraka na rehema zake zisizohesabika ndani ya muda huu na kuongea naye mara kwa mara kwa muda mrefu. Sayyidna Ahmad[as] alimwambia Hadhrat maulvi Abdullah Sanori sb akimuelezea hayo kwamba:

"*Ewe Mian Abdullah! Nimefunguliwa milango mingi ya fadhili kuu za Allah SWT ndani ya siku hizi na muda mwingine, Allah aliongea nami kwa muda mrefu mrefu*." (Siratul Mahdi)

Miongoni mwa fadhila hizo na bishara alizozipata Hadhrat Ahmad[as] ni bishara ya rehema juu ya kuzaliwa kwa Mwana wa Ahadi, ambaye ametajwa ndani ya funuo zake kama Mwana Aliyeahidiwa, Noor ul Allah, Roho Takatifu na Neno la Allah n.k

Kwa kweli ishara hii ni kubwa sana mno, miongoni mwa ishara za kiungu na Sayyidna Ahmad[as] aliieleza ishara hiyo kwa maneno yafuatayo katika tangazo lake la tarehe 20 ya Februaray 1886 kuwa:

"*Amebarikiwa yule ajaye kutoka mbinguni.Atafuatana na rehema ambayo itashuka Pamoja naye. Atahusishwa na utukufu, ukuu, na utajiri. Atakuja duniani na atawaponya wengi wenye maradhi kwa njia ya sifa zake za Umasihi na kwa njia ya baraka za Roho ya kweli. Yeye ni neno la Allah kwani ukarimu na heshima ya Allah imemtuma na Neno la Utukufu. Atakuwa na akili sana mno na ufahamu na atakuwa mpole wa moyo na atajazwa na elimu ya nje na ndani. Atawafanya watatu kuwa wanne.(hii maana yake haikubainishwa). Ni Jumatatu. Jumatatu ilyobarikiwa. Mwana wa kiume, furaha ya moyo, aliyenyanyuliwa, Mtukufu, mdhihirishaji wa Aliye ni wa Mwanzo na Mwisho, alama ya Yule Aliye Mkweli na wa Juu. Kana kwamba Allah ameshuka toka mbinguni. Kufika kwake kutabarikiwa sana sana na kutakuwa sababu ya kudhihirika kwa jalali ya Uungu. Nuru inakuja, nuru hasa , nuru iliyosingwa na Allah uturi wa mapenzi yake. Tutampulizia roho Yetu atahifadhiwa chini ya kivuli cha Allah. Atakuwa upesi upesi katika umbo na atakuwa sababu ya kukombolewa wale walio utumwani. Atajulikana mpaka pembe za dunia na mataifa yatabarikiwa kwa ajili yake. Ndipo atachukuliwa juu mbinguni kwenda mahali alipotayarishwa na jambo hili limekwisha katwa.*"

{Tangazo la tarehe 20 Februari, 1886}.

Kisha aliandika akinukuu funuo kwamba:

"*Rehema itafika pamoja na kuja kwake. Yeye ni nuru na ni mabruk na mtakatifu na yu miongoni mwa watawa. Ataeneza baraka na atawalisha watu chakula safi na atakuwa mwenye kuinusuru dini…. Atakuwa mmoja kati ya ishara zangu na atakuwa Beramu ya misaada yangu ili kwamba wale wanaokukadhibisha wajue ya kuwa mimi niko pamoja nawe kwa njia ya rehema yangu iliyodhihirika…….. Atakuwa na ufahamu na akili na atakuwa mwenye kupendeza. Moyo wake utajazwa elimu, batini yake itakuwa na upole na kifua chake kitajazwa utulivu. Atajaaliwa na roho ya Umasihi na atabarikiwa na roho mwaminifu. Jumatatu,Jumatatu iliyobarikiwa,Roho za watu wenye baraka zitafika kwako*" (Ainae kamalate Islam uk 577-578).

Akiitolea maelezo bishara hii, Masihi Aliyeahidiwa,Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad amani ya Mungu iwe kwake, alisema:

"*Hii siyo bishara tu bali ni ishara adhimu sana mno ya mbinguni ambayo Allah amenionesha kama burhani ya ukweli na adhma ya Mtume aliye ni mpole na mwenye huruma. Muhammmad mteule[saw] amani na baraka za Allah ziwe kwake yeye na ummati wake. kwa hakika ishara hii ni bora, na kubwa na ni afadhali na ni kamilifu na tukufu mara mia zaidi kuliko kumfufua mtu aliyekufa.*" (Majmuae Ishtiharat J.1.UK.99)

Akiendelea kutoa maelezo ya funuo zake zingine zilizomhusu mwana huyu Masihi aliyeahidiwa alieleza:

"*kuzaliwa kwa Mahmood mwanagu mkubwa kulitabiriwa wazi wazi katika Tangazo la kijani Pamoja na jina Mahmood. Tangazo lile lilitolewa Pamoja na utajo wa kifo cha mtoto wa kwanza wa kiume na lilikuwa lenye kurasa nyingi kama kijitabu.* (Dhamima Anjame Atham[1897] uk.15)

Halafu Sayyidna Ahmad[as]alitoa matangazo mengine yenye kueleza zaidi bishara hii iliyo kuu, alisema ya kuwa mtoto huyu atakuwa na majina mengi kama Bashir na Mahmood na mengineyo. Pia aliambiwa na Allah ya kuwa mtoto huyu atazaliwa katika muda wa miaka 9 tangu siku ya kutangazwa habari hii ya ghaibu yaani tangu tarehe 20 February 1886.

Sayyidna Ahmad[as] aliandika: "*Katika tangazo langu la tarehe 20 February,1886 mna bishara ya kuzaliwa mtoto wa kiume mwema ambaye atakuwa na sifa zilizotajwa ndani ya tangazo hilo. Mwana huyu, sawa na ahadi ya mbingu atazaliwa katika muda wa miaka tisa mapema au mwishoni lakini bila shaka ni katika muda huo.* (Tangazo la tarehe 22 Machi,1886

Endelea uk. 4

Bishara kumhusu Mwana Aliyeahidiwa[ra]

Kutoka uk. 3

Tablighe Risalat J.1)

Kisha alisema akisisiteza zaidi kuhusu muda kuwa: "*Sawa na ahadi ya mbingu mwana huyu atazaliwa bila shaka katika muda uliotangazwa. Mbingu na ardhi zinaweza kuondoka lakini ahadi ya Allah kamwe haiwezi kukosa kutimia.*"

(Tablighe Risalat J.1.uk.127) halafu alisema kwa kutilia mkazo kwamba: *Kama kumebaki siku moja tu ya muda uliotangazwa, basi Allah, Bwana wa heshima na Utukufu, Hataiacha siku ile ipite mpaka Atimize ahadi Yake.* (Tangazo la tarehe 12 Januari 1889. Tablighe Risalat J.1.uk.148)

Sawa na funuo na bishara hizo mwana huyu alizaliwa ndani ya muda uliotanzawa mnamo 12 Januari 1889 na kupewa jina tukufu la Mirza Bashir ud din Mahmood Ahmad[ra] kisha hakuzaliwa mtoto mwingine katika muda huo wa miaka tisa. Kisha mwana huyu wa ahadi alichaguliwa kuwa khalifa wa pili wa Sayyidna Ahmad[as] mnamo 1914 baada ya kufariki kwa khalifa wa kwanza Hadhrat hakim maulana Noor Uddin[ra]

Tunaweza kupima jinsi ilivyo kuu Bishara hii kama ingekuwa tu ya kuwa imetolewa bishara yam toto wa kiume atakayepata umri mrefu hata hivyo ingelikuwa ni Habari kubwa sana, maana hapana aliye na Habari kamili ya kuwa yeye na mkewe wataishi muda wa miaka tisa kisha watapata mtoto wa kiume ambaye atapata umri mrefu lakini Habari hii haikuishia hapo bali sifa zilizotukufu za mtoto huyu pia zilitajwa na jambo hili haliwezikani kwa mwanadamu. Kurani Tukufu (72:27-28) na vitabu vingine vya dini zingine zinatoa Ushahidi ya kuwa ajuaye mambo ya ghaibu ni Allah tu na mtu hawezi kusema maneno yoyote yakatimia ila anapoambiwa na Allah. Sayyidna Ahmad[as] mwenyewe alitilia mkazo sana Bishara hii na akasema ya kuwa bishara hii itakapotimia itaonekana ya kuwa bila shaka Allah anasikia dua za waja wake na anawapasha Habari za ghaibu na pia alisema ya kuwa kutabiri kuzaliwa kwa mtoto mwenye sifa hizo kwa hakika ni jambo lenye adhma sana ambalo lahakikisha kuwapo kwa Allah na ya kuwa Yeye Mungu ni Mwenye uwezo wa ajabu.

Kama tumeshajua kuwa bishara hii ni ishara kuu ya kimbingu kwa sababu ndani ya bishara hii mlibebwa lundo la bishara nyingine ambazo baadhi yake ni yafuatayo kwa ufupi:

x. Kwamba Masihi aliyeahidiwa atapata mtoto wa kiume, nay a kwamba
x. atakuwa mwenye umri mrefu,
x. Mtoto huyu atazaliwa ndani ya muda wa miaka tisa toka siku ya kutangazwa kwa Bishara hiyo
x. Mtoto huyu atakuwa mbegu ya Masihi Mwenyewe
x. Mtoto huyu atakuwa mtakatifu sana
x. kwamba atakuwa na majina Imanueli Bashir na Mahmood
x. Kwamba Atahusishwa na Utukufu, ukuu na utajiri
x. atadhihirisha heshima, utukufu wa Kurani Tukufu
x. Kwamba atakuwa mwenye kuwaponya wenye maradhi
x. kwamba atakuwa na akili sana mno na ufahamu mkubwa
x. ya kuwa Atakuwa mpole wa moyo
x. Atajazwa na elimu ya nja na ya undani
x. Atawafanya watatu kuwa wanne
x. Ya kuwa kuja kwake kutaleta baraka na ushindi wa haki
x. kwamba kuja kwake kutadhihirisha utukufu na jalali ya Allah hata itaonekana kana kwamba Allah Mwenyewe Ameshuka kutoka juu
x. Ya kwamba mtoto huyu atahifadhiwa na kulindwa na Mungu
x. kwamba atakuwa haraka haraka
x. Ya kwamba atakuwa sababu ya kukombolewa mataifa yaliyo utumwani
x. na mataifa yatabarikiwa kwake
x. Ya kwamba atajulikana mpaka pembe zote za Dunia
x. Ya kwamba atainusuru Imani ya Islam
x. ili wajue kuwa Mungu yu Pamoja na Masihi aliyeahidiwa
x. kwamba amepewa roho takatifu na kuepushwa na uchafu wowote
x. Mtoto huyu ni nooru ya Allah
x. kwamba atakuwa Neno la Allah
x. Ya kwamba atakuwa miongoni mwa ishara za Mungu
x. Ya kwamba atakuwa Berau ya misaada ya Mungu ili wamkadhibishao Masihi wajue kuwa Mungu yu Pamoja naye.

Jinsi ilivyotimia Bishara hii kuu

Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad[ra]khalifa wa pili wa Sayyidna Ahmad[as] alioteshwa njozi na Allah Mnamo tareh 4 ya January 1944 alipokuwa mjini Lahore na kufunuliwa kwamba yeye ndiye Mwana Aliyeahidiwa aliyetajwa ndani ya bishara ya Sayyidna Ahmad[as] ya tarehe 20 February 1886. Hadhrat Khalifa tul Masih wa pili[ra] aliporejea Qadian mara baada ya kupata ufafanuzi huo kutoka kwa Allah basi alitangaza mnamo tarehe 28 Januari 1944 akiwa Masjid Aqsa Qadian na kusema: "*Mimi ndiye nitimizaye bishara hiyo kumhusu mwana aliyetabiriwa.*"

Jumuiyya iliandaa mikutano ya hadhara mnamo 1944 katika miji mikubwa mikubwa ya India kama Hoshyarpur, Lahore, Ludhyana na Dehli kwa ajili ya kuadhimisha kutimizwa kwa bishara hiyo ya Hadhrat Ahmad[as] na Khalifatul Masih wa Pili Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad alishiriki mwenyewe na kuwahutubia wanajamaaat ndani ya mikutano hiyo na kufafanua akibainisha njozi yake kuwa: Mimi nasema nikimshuhudhisha Allah kwamba nilipata kusema kwenye njozi kwamba;

"*Anal Masihul Mau'du Masiluhu wa Khalifatuhu*"

(tafsiri: mimi ni Masihi Aliyeahidiwa, yaani mwano wake na Khalifa wake) basi ninatanga kutokana na amri ya Allah tena kwa kuapa kabisa kwamba Mweyezi Mungu Amenijaalia kuwa Mwana Aliyeahidiwa wa Sayyidna Ahmad[as] ambaye atafikisha ujumbe wake hadi pembe zote za dunia.

Tunapata kufahamu vyema kabisa kuyapitia maandiko ya Sayyidna Ahmad[as] kwamba bishara hii si kwa ajili ya kupata mwana tu bali ni bishara kuu inayomhusu:

Mwana Adhimu, Mwema sana, Mtakatifu, Mwenye akili nyingi na ufahamu mkubwa, Mwenye hekima na busara zaidi, mwenye kupata umri mrefu, atakayejazwa na elimu ya nje na ndani. Kuja kwake ni kama Allah Ameshuka kutoka mbinguni, kufika kwake kutabarikiwa sana mno na kutakuwa sababu ya kudhihirika kwa Jalali ya Uungu. Atakuwa Nuru hasa, nuru iliyosingwa na Allah uturi wa mapenzi Yake, atajaaliwa na roho Takatifu na kuhifadhiwa chini ya kivuli cha Allah. Atajulikana mpaka pembe zote za dunia na mataifa yatabarikiwa kwa ajili yake.

Hebu niambieni kama mtu yeyote anaweza kutoa bishara ya namna hii juu ya mwanaye ambaye hajazaliwa! Kwa kweli kabisa bishara hii ni kubwa sana wala haijapatikana mfano wake katika dunia hadi leo hata kwenye historia ya manabii wote watukufu ila bishara hii imetolewa na mbora wa manabii woote na kuelezwa na Masihi na Mahdi Wake, amani, rehema na baraka ziwe juu yake. Aamin.

Hadhrat khalifa tul Masih wa pili anasema:

Mimi ambaye Allah amenijaalia mwenye kusadikisha na kuitimiza bishara hiyo, ninatoa tanbihi na kuwaita maulamaa (masheikh) wote kwa ajili ya kuandika maelezo ya sehemu yoyote ya Kurani na kupata msaaada wa watu wengi wingine wawezao na vitabu vingi lakini mimi nitapata ushindi kwa fadhila za Allah na alieleza mara kadhaa kuwa nime fundishwa na Mungu Mwenye Enzi tafsiri, maarifa na maelezo mazuri na mapya ya Kurani Tukufu na maelfu ya madhmuni ya dini na hakuna awezaye kunishinda katika uwanja huu.

Vitabu vyake, hotuba zake zinatoa Ushahidi wa kutosha juu ya hayo ila ningependa kuweka mbele ya wasomaji wetu "Tafsir e Kabiir" pekee kwamba hadi leo hii ni changamoto kwa ajili ya wataallamu, maulamaa na kwa watu wote kwa jumla kuwa je, kuna mtu yeyote anayeweza kuandika mfano wake?

Bali nimekumbuka ushuhuda wa mwanazuoni anyeitwa, Allama Nyaz Fateh Puri aliyemuandika Khalifa wa Pili, baada ya kuisoma Tafsire Kabiir kwamba:

"*Hakuna shaka kwamba wewe umebuni mfumo mpya wa kuisoma Kurani Tukufu na tafsiri hii (maelezo) ni tafsiri mpya kabisa kwa namna yake ambayo umethibitisha kwayo kwa uzuri mkubwa kuwa akili na sayansi vinakuenda Pamoja. Elimu yako ya juu, akili yako iliyopana sana, ufahamu wako na busara isiyo ya kawaida na uzuri wako wa kulithibitishia jambo ni vitu vinayodhihirika kwa kila neno. Nasikitika sana kwamba kwa nini nimeghafilika nayo hadi sasa.* (Sawaneh Fazle Umar J.3.UK.163)

Mwana huyu wa ahadi alifundishwa na Malaika wa Allah maelfu ya madhumuni yahusuyo Qur'an na Dini na kupata funuo na wahi nyingi za Allah[swt] moja kwa moja na kujifunza elimu ya Kutani tukufu.

Safari moja, Hadhrat Musleh Maud[ra] alisema kuwa:

"*Nami pia nimefundishwa maarifa ya Kurani ambayo kwayo naweza kumjibu yeyote, atakayeailisha Kurani hata kama anajua elimu yoyote au mfuasi wa dini yoyote, kwa Fadhili za Allah nitamjibu kuipitia Kurani tu, Nimetoa tanbihi hiyo mara kadha kwa watu kwamba waandike maarifa ya Kurani kushindana nami.. lakini hakuna aliweza kujitokeza… pia ninadai kuwa nitaeleza maarifa mapya ya Kurani.*"

Kisha alisema:" *Mimi, ambaye Allah Amenijalia, mwenye kuitimizia bishara (hiyo ya Musleh Maud[ra]), ninawatangazia maulamaa wote kwamba waandike maelezo ya sehemu yoyote ya Kurani kushindana nami na wapate msaada kwa yeyote na vitabu vyovyote lakini hata hiyo nitashinda mimi tu kwa Fadhili za Allah.*" (Al-Fazal 23 April 1944)

Vitabu vya Mwana Aliyeahidiwa vinavyozidi 100 ni dalili bayana kuwa yeye ana daraja la pekee katika kutoa maelezo ya Kurani Tukufu kisha jambo hili limeelezwa na wapenzani wake pia kama alivyosema Maulana Zafar Ally Khan aliyekuwa mhariri wa gazette kwamba:

Haya yanathibitisha wazi kabisa kuwa Sayyidna Ahmad[as] alikuwa na yakini kamili, sawa na bishara ya Allah kwamba, mtoto huyu aliyeahidiwa atakuwa kizazi chake yeye mwenyewe, atakuwa wakiume, atazaliwa ndani ya muda wa miaka tisa tu, atakuwa mwenye umri mrefu na si tu mwenye kufuata dini yake bali atakuwa sababu ya kudhihirisha ukweli wake na kueneza dini yake kwenye pembe zote za dunia na atakuwa na sifa zote zile ambazo zimebainishwa ndani ya funuo zake ambazo tumeshaziandika hapo. Sasa je, kuna mtu yeyote awezaye kutoa bishara ya namna hii kwa kumzuilia Allah? Kisha kama atatunga uwongo juu ya Mungu basi Allah Atamsaidiaje hadi kumjaalia na mtoto atakayepata mafanikio makubwa na mazuri ya pekee kama alivyopata mwana huyu na mafanikio yake yanakubaliwa na hata maadui yake! Ningependa kuweka mbele ya wasomaji wetu watukufu ushuhuda wa mwanazuoni aliyekuwa adui wa Mwana Aliyeahidiwa[ra] kwa ajili ya tofauti ya Imani, maulana Zafar Ally Khan, yeye anasema akiwaelezea wenzake waliokuwa wapinzani au maadui wa Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad[ra] kwamba:

Sikilizeni vizuri! Nyinyi na wenzenu, hamwezi kushindana na Mirza

Inaendelea uk. 5

Kambi ya Malezi mkoani Simiyu na Darasa la Malezi mkoani Mara

Na **Sh Ali Dino Tahir - Simiyu**

Sawa na maagizo ya Amiri na Mbashiri Mkuu wa Jumuiyya ya Waislam Waahmadiyya - Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry sahib, kambi ya malezi ilifanyika kwa siku 8, mkoani Simiyu kuanzia tarehe 14 Disemba 2021.

Kambi ya malezi ilifanyika kwa siku 4 za mwanzoni kwenye tawi la Kisisa halafu kwenye tawi la Ntobo kwa siku 4 za mwisho na Khuddam na Atfal walitembea kwa miguu kilomita 6 na kufika katika eneo husika.

Kikao cha ufunguzi wake kilihudhuriwa na Sheikh wa Mkoa, Rais wa Mkoa na Walimu sita wa matawi mbali mbali. Wakina mama waliweza kutoa mchango mkubwa kwa ajili ya kuwapikia chakula n.k. ambao wanastahili maombi yetu, Mwenyezi Mungu Apokee juhudi zao na kuwalipia malipo mema kutoka kwake. Aamina.

Watu 150 walihudhuria kambi wakiwemo 94 Khuddam na Atfal,
24 Nasirat, 6 Walimu na 26 wazazi na viongozi.

Masomo yaliyofundishwa

Khuddam, Atfal na Nasirat walifundishwa matini ya sala pamoja na tafsiri yake na Atfal 12 na Nasirat 4 waliweza kumaliza tafsiri ya sala yote.

Atfal na Khuddam, walifundishwa maswali na majibu 300 kutoka *Masomo ya Dini* na kufanyiwa mashindano baina yao siku ya mwisho.

Hotuba mbalimbali pia zilitolewa na wataallamu kuhusu mada kama:

1.Hoja za kuthibitisha Uwepo wa Mwenyezi Mungu,
2. Maelezo muhimu juu ya unabii na ukhalifa na kujibu maswali ya washiriki.
3. Kupigana Jihadi na vita vya Kiislam na majibu ya shutuma za wapinzani
4. Maombi ya Mtume Mtukufu^{saw}
5. Maisha matakatifu ya Mtume^{saw}
6. Maisha ya Nabi Issa^{as} na mama yake^{ra}
7. Matukio mbalimbali yenye kusisimuaimani kutoka katika Maisha ya Hazrat Masih-e-Maud^{as} na makhalifa wake watukufu
8. Maswala ya Fiqhi kuhusu sala, Udhu'u na Tayammamu
9. Baraka za kusoma Qur'an Tukufu
10. Baraka za kujitolea mali n.k.

Hafla ya kufunga kambi, ilifanyika tarehe 20 Disemba, na kuhudhuriwa na waheshimiwa wengi na kugawa zawadi kwa washindi mbali mbali kwenye mashindano ya kielimu na kimwili na hafla hii tukufu ilifungwa na dua ya Pamoja.



Wahudhuriaji wa Darasa la Malezi wakitazama Hotuba ya Huzur^{atba}

Darasa la Malezi kwa siku 7 Mkoani Mara

Kwa fadhila za Allah, uongozi wa mkoa wa Mara uliweza kuandaa darasa la malezi kwa Khuddam na Atfal ambalo lilianza tarehe 2 Januari 2022 na hafla ya ufunguzi ilianza kwa kusoma Qur'an Tukufu, kusoma mashairi yaliyofuatiwa na hotuba mbili za wataallamu.

Wakinamama waliweza kuwasaidia washiriki wa kambi hiyo kwa kuwapikia chakula n.k, tunawatolea shukrani nyingi kwa msaada huo.

Mahudhurio yalikuwa: 62 kwa ujumla, wakiwemo 42 khuddam na Atfal,
7 Nasirat, 5 walimu na 8 wazazi na viongozi.

Khuddam, Atfal na Nasirat walifundishwa sala, tafsiri ya sala na Atfal 8 waliweza kuhifadhi tafsiri kamili ya sala pamoja na Nasirat wawili.

Hotuba mbalimbali juu ya malezi zilitolewa kama:

- Sala na adabu zake
- Utambulisho wa Jamaat
- Maisha ya Mtume mtukufu^{saw}
- Nidhamu ya Jamaat na Baraka za Ukhalifa
- Maswala ya Kifiqhi kuhusu sala, Udhu na Tayammum
- Baraka za Ucha-Mungu na Elimu.

Bishara kumhusu Mwana Aliyeahidiwa^{ra}

Kutoka uk. 4

Bashiruddin Mahmood hadi siku ya Kiyama kwani Mirza Mahmood anayo elimu ya Qur'an na ninyi mna kitu gani?... Mirza Mahmood anayo jumuiyya inayoweza kujitolea heshima yao, mali zao na nafsi zao kwa dokezo lake moja tu…Mirza Mahmood anao wabashiri, wataaallamu wa elimu mbali mbali. Yeye (Mirza Mahmood^{ra}) ameshapeperusha bendera yake kwenye kila nchi." (Aik Khofnak Sazish, Kalamullah ka Martaba aur Muleh Maud uk.164-165)

Safari moja Hadhrat Khalifatul Masih wa Nne^{rh} alisema akiwahutubia wanajamaat kwamba: *"Kila mmoja wenu, akiwa mwanaume au mwanmke ajisogeze mbele kwa ajili ya kuiga sifa ambazo zimeelezwa katika bishara ya Mwana Aliyeahidiwa, hivyo basi ninapowaambieni kwamba muwe musleh maud (wenyewe) na wakubwa wenu wawe musleh maud na wadogo zenu pia wawe musleh maud, wanaume wenu pia wawe musleh maud na wanawake wenu pia wawe musleh maud lakini sisemi kamwe kwamba mupate tamaa za madaraka ya juu, bali ninasema hii kwamba mumwombe Mola wenu kwa ajili ya kupata sifa zile zinazohitajika leo kwa ajili ya kuhuisha binadamu wa zama hizi…. Haiwezikani kuihuisha dunia leo bila kujipatia sifa hizo….mujaribu kuwa Musleh maud kwa maana hiyo na kadri mnavyoweza kupata uwezo huu basi muendelee kumyenyekea Mungu zaidi na zaidi.*" (Jarida la Khalid, la Februari 1991)

Ningependa kumaliza kwa maneno yafuatayo ya khalifa wetu wa zama, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad^{atba} yeye anasema:

"Basi leo hii tunawajibu huu kwamba tujaribu kuwa Musleh maud sawa na uwezo wetu. Tueneze ujumbe mzuri wa Islam kwenye kila kona kutokana na elimu yetu, kauli yetu na kitendo chetu. Tueleke kwa ajili ya kujirekebisha na kuirekebisha jamii yetu pia. Na tujaribu sawa na uwezo wetu kwa ajili ya kudumisha mageuxi na ujumbe ulioletwa na Mtume Mtukufu^{saw}, hivyo basi kama tutakuwa wenye kupitisha Maisha yetu kwa wazo la namna hii ndipo tutakuwa wenye kutekeleza wajibu wetu wa kuadhimisha siku ya Mwana Aliyeahidiwa wala hotuba zetu zitakuwa zinaenda bure tu. Allah Atuwezeshe kwa ajili ya hilo."(Hotuba ya Ijumaa ya 18 Februari 2011)

Uchawi - Imani za kishirikina

Kutoka uk. 1

mfungulie maarifa na elimu ya Qur'an] sasa basi tunaona kuwa kudhihirisha batili katika sura ya haki ni uchawi. Hizo ni maana za wazi kuhusu neno uchawi hivyo tunajifunza kuwa uchawi si kitu chenye nguvu za kisiri na kuweza kumloga mtu , bali ni udanganyifu wa kielimu kuhusu kitu Fulani na kukifanya watu wakione tofauti.

Neno hilo sio kila mara liwe na tafsiri ya mchawi pia lina maana sita zingine zinazo patikana kwenye kamusi ya Akrab na Lane.

Neno hili limetumika mara 42 ndani ya aya 41 za Quran likiwa na maana tofauti tofauti na InshaAllah nitaeleza baadhi tu ya aya ili kuweka wazi zaidi na hasa wakati wa kuwafahamisha Waislam juu ya imani hii ya ushirikina.

Aya ambazo neno sihir au saahir limetumika ni hizi zifuztazo [2; 10] [5; 111] [6;8] [7;110] [7;114] [7;117] [7;121] [7;133] [26;154 na 186] [61;7] [74;25] hizi ni chache tu kati ya aya 42 nilizo zitaja.

LILIVYO TUMIKA NDANI YA QURAN.

Neno hili lilivyo tumika ndani ya Quran lime maanisha uongo ,udanganyi ,ughiribu na hasa pale nabii wa Allah anapo tumwa kwa watu na kuwaeleza ishara Fulani ushahidi una patikana katika Quran kuwa wao walipo waambia watu wa mwamini mungu waka anza kuwaita wao wachawi. Mfano sura ya 61;7 Na alipo sema Issa mwana wa Mariam; Enyi wana wa Israeli ,mimi ni Mtume wa Allah kwenu ,ni sadikishaye yaliyo mbele yangu katika taurati na kutoa habari njema ya Mtume atakaye kuja nyuma yangu jina lake ni Ahmad ; lakini alipo wafikia kwa ishara zilizo wazi,wakasema huu ni udanganyifu dhahiri. 10;77-78 Basi ilipo wafikia haki kutoka kwetu wakasema; huu ni uchawi dhahiri. Akasema Musa ; Je mnasema hivi juu ya haki ilipo wafikieni, Je huu ni uchawi? Na wachawi hawastawi[yaani hawafaulu] 10;81-82 Basi walipofika wachawi ,Musa akawaambia; Tupeni mnavyo taka kuvitupa. Na walipo vitupa, Musa akasema; mlivyoleta ni udanganyifu tu wa macho; hakika Allah hivi karibuni Ataubatilisha. Hakika Allah Hastawishi vitendo vya waharibifu 20;70-71 Na kitupe kilicho katika mkono wako wa kuume; kita vimeza walivyo vitengeneza; hakika wametengeneza hila za mchawi hata faulu popote. Basi wachawi waka angushwa kusujudu, wakisema, Tume mwamini Mola wa Harun na Musa.

NUKTA KADHAA ZA KUKUMBUKA HAPA

1 Katika sura ya 61 aya ya 8 ime elezwa kwamba pindi alipo wajia kwa ishara zilizo wazi waka sema huu ni udanganyifu dhahiri, kwa nini waseme udanganyifu ;kwa sababu hawakuelewa ishara zile kwa kung'ang'ania mila zao za zamani na kuchukua mambo yao ya udanganyifu kwa njia mbalimbali

Endelea uk 11

Bustani ya Washairi

KWA HERI NI WETU BWANA

Ramadhani wetu bwana, kwa wema uliingia
Nasi tulishikamana, kwa wema kukupokea
Tlifunga kwa dhamana, kwa fadhila za Jalia
Kwa heri ni wetu bwana, Majaliwa kuonana

Nyoyo zilitakasika, kwa kuzileta fadhila
Na mbaya alidhikika, kimya akamba kulala
Shetani ni msifika, kwa ubaya wa mikwala
Kwa heri ni wetu bwana, Majaliwa kuonana

Ulimwengu hutulia, ukakunywa kama tao
Wa hii yetu dunia, yalisha majaribio
Kila mja alilia, na kumsaka kwa mbio
Kwa heri ni wetu bwana, Majaliwa kuonana

Usiku tulisimama, Manani kumlilia
Tulikimwomba Karima, mema kutuzidishia
Mabaya yapate koma, sote tupate tulia
Kwa heri ni wetu bwana, Majaliwa kuonana

Ramadhani mtajika, karibu tena mwakani
Mola wetu Msifika, Atujalie mwakani
Tufikie kwa hakika, tuyapate ya Manani
Kwa heri ni wetu bwana, Majaliwa kuonana

Shukurani nazitoa, kunijalia kufunga
Kwake nikaelekea, kaongeza wake mwanga
Wemawe kanitolea, na mabaya kunikinga
Kwa heri ni wetu bwana, Majaliwa kuonana

Kaditama nimefika, sio mwisho wa kuomba
Uyaondoe mashaka, tupate nyoyo kuwamba
Utulivu kuuweka, kama ngozi yake mamba
Kwa heri ni wetu bwana, Majaliwa kuonana

Harun R. Bundala
S.L.P. 54, Tabora

SUBIRA

1. Ulimwengu sio wangu, nataabika
Yote mipango ya Mungu, ninatomboka
Wala siko peke yangu, kwenye mashaka
Siijui kesho yangu, nitafikaje?

2. Usiku wangu mrefu, usioisha
Humu ndani ya jokofu, mmenichosha
Ninamuomba Turufu, hatanifisha
Siijui kesho yangu, nitafikaje?

3. Na bado nina subira, navumilia
Nitaupata ujira, ninawambia
Moyo hauna papara, umetulia
Siijui kesho yangu, nitafikaje?

4. Siijui kesho yangu, sina hakika
Mungu kimbilio langu, atakumbuka
Maisha yangu machungu, nimegubikwa
Siijui kesho yangu, nitafikaje?

5. Pamoja na hayo yote, ninakumbuka
Sala ninasali zote, siweziruka
Ninapopata chochote, namkumbuka
Siijui kesho yangu, nitafikaje?

6. Kuna muda ninalia, kama mtoto
Mangumu ninapitia, bila majuto
Na Mungu ninamwambia, mambo mazito
Siijui kesho yangu, nitafikaje?

7. Naendeleza subira, nimenyooka
Ninazisaka ngawira, nitazishika
Naomba bila bakora, ninahenyeka
Siijui kesho yangu, nitafikaje?

8. Na kinachonishangaza, wanaumia
Na wanapata bughudha, kunisemea
Mwenyewe bado nakaza, yatatimia
Siijui kesho yangu, nitafikaje?

9. Chakula changu cha shida, navumilia
Ninashindwa kujidoda, nimepotea
Huwa sinywi hata soda, nawaambia
Siijui kesho yangu, nitafikaje?

10. Nakubali kila hali, nayopitia
Bado ninajikubali, mia kwa mia
Itakwisha hii hali, nangojelea
Siijui kesho yangu, nitafikaje?

11. Tuko watu wengi sana, wenye majanga
Hata kama mkinuna, nakujitenga
Ewe Mungu wangu ona, wananinanga
Siijui kesho yangu, nitafikaje?

12. Nimefikia mwishoni, kuwakumbusha
Nyi wote nduguzanguni, sijapotosha
Usiombe we ni nani, wajizungusha
Siijui kesho yangu, sina mashaka.

Abdallah Kalindima (Chuma Chakavu)

KIPIMO CHA UCHAMUNGU

1. Ukweli nauwandika, Akili inanituma,
Jaribu kuyaepuka, Ili upate heshima,
Uwasi kuuepuka, Utufike mwisho mwema,
Kipimo cha uchamungu, Majaribu ya dunia.

2. Shikamana na sheria, Mwenyezi katuwekea,
Kuzingatia sheria, Amri katuwekea,
Ole ldvunja sheria, Adhabu katuwekea,
Kipimo cha uchamungu, Majaribu ya dunia.

3. Yatakuvunja imani, Haki utaangamia,
Usijivishe mwilini, Maradhi ya kuumia,
Yatakuvunja imani, Mwishowe kuangamia,
Kipimo cha uchamungu, Majaribu ya dunia.

4. Vipimo naviandika, Tega sikio sikia,
Usikiapo epuka, Jiweke mbali sikia,
Usivutike hakika, Kuwa imara sikia,
Kipimo cha uchamungu, Majaribu ya dunia.

5. Huyashona mavazi, Yakubana kuvutia, Na yale mabega wazi, Kifuwa kutuvutia,
Na siket'i za uwazi, Kila kona zapitia,
Kipimo cha uchamungu, Majaribu ya dunia.

6. Wanatuweka kitanzi, Kuitamani dunia,
Tujihadhari wapenzi, Tusitamani dunia,
Mbele ya ola
Kipimo cha uchamungu, Majaribu ya dunia.

Madumula Ng'amilo

WAKATI NDIO HUSEMA

Naanza kwa jina Lako, Ewe Mola mtukuka
Ambaye kwa sifa zako, hakuna anayefika
Afananaye hayuko, kwa wote waloumbika
Wakati ndio husema, si hekima zake mtu

Wakati huu tuliko, Islam yatikisika
Tena haina mashiko, pote yaweweseka
Mamlakani waliko, hawajui pa kushika
Wakati ndio husema, si hekima zake mtu

Katika hili zumbuko, Imam ahitajika
Wa kuipa imariko, dini ya Mola Rabuka
Aondoe choko choko, za wapendao faraka
Wakati ndio husema, si hekima zake mtu

Wakati hutoa mwako, nini kinahitajika
Sawa nalo dhihiriko, ya uma ulipofika
Sababu ya maanguko, husema limepasuka
Wakati ndio husema, si hekima zake mtu

Elimu dini haiko, dhana kasi imeshika
Yamebaki maandiko, maana imetoweka
Visa ndio la shiko, washindana kutamka
Wakati ndio husema, si hekima zake mtu

Wa kuongoza hayuko, kwa wote akasikika
Hivyo kuna mpasuko, wa dini yake Rabuka
Na hilo ndio anguko, Islam imefika
Wakati ndio husema, si hekima zake mtu

Mimi nawapa kumbuko, Mtume alitamka
Mia miaka kamiliko, Mujadid atafika,
Na dini yenye sumbuko, lazima taimarika
Wakati ndio husema, si hekima zake mtu

Hassan Sango
Jang-e-Muqaddas kwenye karatasi

MUNGU WETU HANA DINI

1. Ndugu zangu habirini, wenye dini wapagani
Sikio niazimeni, mungu wetu hana dini
Chuki sababu ya dini, hutookoka motoni
Mapenzi yawe kwa wote, bila chuki kwa yeyote

2. Mmoja ulimwenguni, ndiye muumba wa wote
Mungu wa duniani, sayari na nyota zote
Mungu wetu hana dini, habagui vyake vote
Vilivyoko aridhini, hata vya mbinguni vyake

3. Vyakuvila aridhini, wanyama nayo mimea
Hewa maji duniani, kila kitu cha tumia
Mungu wetu hana dini, tuache kujibagua
Kila kitu limwenguni, mahitaji akatoa

4. Ubora ulimwenguni, binadamu akapewa
Atawale vya mbinguni, na akili akapewa
Mungu wetu hana dini, tutumie tulopewa
Sigombane kisa dini, utu ukapuuziwa

5. Akaiweka na dini, Ili tuweze mtambua
Dunia iwe amani, kila kiumbe tulia
Mungu wetu hana dini, kazi kwetu kumjua
Dini hasa ni amani, salama kuwa dunia

6. Utulivu duniani, upendo na usalama
Ndilo hasa dhumuni, yakujitendea wema
Mungu wetu hana dini, humpenda alomwema
Una dini mpagani, wengine wawe salama

7. Acha nifike mwishoni, akili mekufunguw,
Mungu wetu hana dini, acheni kujibaguwa
Kama kafiri kwa dini, kimaisha takutowa,
Tupendane bila dini, kituacha metugawa

Masihi Omary Stambuli

YAKINI

Kikombe kimetakata, kwa nje kinavutia
Kwa kila anayepita, mate anakimezea
Na mimi ningekipata, fuadi ingetulia»
kumbe siri ya maiti, aijuae muosha!
Pamwe na mshika kata, maji anayemwagia
Kimya huwa ana sita, lolote kujisemea
Kila mpenda kubwata, kichwani zimepungua
Akatula omungoma, kamanywa omubambi

Uzuri wenye kumeta, ni ndani kuchungulia
Yaliyomo ni mafuta, au uchafu ajaa
Bila yakini tajuta, katika hino dunia
Tizama nje na ndani, kuupata utulivu

Kaditama hujapata, bileshi wajisumbua
Yakubidi kujikita, kiini kukifikia
Au utaula mwata, janga utajivunia
Na kila mvuna janga, hula pamoja na wake

Mahmood Hamsin Mubiru (**Wa Mamba**)
Kiwalani - Migombani

DUA MWANANA

Ya Rabi nifunze Kina, sifa nisizizoee
Nipe nguvu za Ujana, Na akili za Mzee
Na hekima za Ujana, Uwezo wa Kipekee
Kwa marefu na mapana, Maovu niyakemee
Kwa Kazi zenye mwanana, Na malengo nifikie

Shabani A. Shunda
Shunda Mshundia Wana - Daluni Tanga

Punda na Chui

Punda alimwambia simbamarara: "Nyasi ni bluu".

Chui akajibu: "Hapana, nyasi ni kijani."

Mjadala ukawa mkali, na wawili hao wakaamua kuwasilisha suala hilo kwa simba, Mfalme wa Pori.

Kabla ya kufika kwenye eneo la msitu ambapo simba alikuwa ameketi kwenye kiti chake cha enzi, punda alianza kulia: "Mtukufu, eti ni kweli



kwamba nyasi ni za bluu?".

Simba akajibu: "Kweli, nyasi ni bluu".

Punda alikimbia mbele na kuendelea: "Chui hakubaliani nami na ananipinga na kuniudhi tafadhali mwadhibu".

Kisha mfalme akasema: "Chui ataadhibiwa kwa miaka 5 ya ukimya".

Punda aliruka kwa furaha na akaenda zake, akiwa ameridhika na kurudia: "Nyasi ni bluu"...

Chui alikubali adhabu yake, lakini akamuuliza simba: "Mtukufu mfalme, kwa nini umeniadhibu, hata hivyo, nyasi ni kijani?"

Simba akajibu: "Kwa kweli, nyasi ni kijani."

Chui akauliza: "Kwa nini unaniadhibu?"

Simba akajibu: "Adhabu haina uhusiano wowote na swali la kama nyasi ni bluu au kijani. Adhabu ni kwa sababu wewe kiumbe shujaa na mwenye akili unapoteza muda kubishana na punda halafu uje kunisumbua kwa swali la kipuuzi".

Fundisha wale ambao wako tayari kujifunza, badala ya kubishana na wale wasio tayari.

TAFUTA MANENO

Yatafute maneno hapo chini kwa kuyazungushia na Penseli

Mkandarasi	Batilisha	Afriti	Taawili
Mfululizo	Hamkani	Henzirani	Tarafa
Masanamu	Istikharaa	Abunuwasi	Istihzaa
Sambaa	Ishaat	Tarakilishi	Maumbile
Mwenyezi	Muhkam	Majlis	Tahariri
Tengemaa	Muutasila	Ngenga	Ghera

T	M	M	T	T	A	R	A	K	I	L	I	S	H	I	G	F
A	T	A	A	H	E	N	Z	I	R	A	N	I	A	K	K	B
H	A	Y	S	J	V	G	T	E	J	T	F	I	B	T	F	B
A	A	S	C	A	L	R	L	A	N	N	Z	C	U	M	F	M
R	W	A	L	N	N	I	C	H	R	E	M	D	N	K	R	U
I	I	M	R	T	B	A	S	B	Y	A	D	H	U	L	I	U
R	L	B	Y	M	N	H	M	N	A	F	F	T	W	S	L	T
I	I	A	U	M	C	T	E	U	A	T	A	A	A	P	R	A
F	Y	A	K	Y	D	W	N	G	G	A	I	R	S	L	I	S
M	M	M	X	D	M	H	N	M	R	H	A	L	I	T	D	I
H	U	T	E	N	G	E	M	A	A	D	E	N	I	X	R	L
A	W	H	K	T	G	W	H	D	N	Y	B	R	R	S	Z	A
M	J	M	K	N	T	K	T	A	Y	Y	F	F	A	T	H	N
K	R	K	L	A	I	B	K	W	M	A	Z	R	K	Y	W	A
A	P	D	W	T	M	M	Y	T	I	S	T	I	H	Z	A	A
N	G	J	S	J	I	S	H	A	A	T	Z	P	Y	Q	Y	K
I	D	I	W	H	M	F	U	L	U	L	I	Z	O	H	T	J

UNGANISHA NUKTA

Unganisha nukta ili upate picha moja iliyokamilika.

Jinsi ya kupika Tambi za Dengu

Na **Mtandao**



MAHITAJI

1. Unga wa dengu ½ kilo
2. Binzari nyembamba ½ kijiko cha mezani
3. Unga wa pilipili manga kijiko 1 cha chai
4. Unga wa mchele ¼ kilo
5. Chumvi kiasi
6. Mafuta ya kula ½ lita
7. Baking powder

JINSI YA KUPIKA

1. Changanya unga wa mchele pamoja na ule wa dengu. Kisha chukua nyunyuzia baking powder na baadaye chumvi. Weka unga wa binzari nyembamba na pilipili manga.
2. Baada ya hapo changaya vizuri na kisha weka maji kidogo kidogo huku ukiukanda hadi liwe donge gumu kama unavyofanya kwenye maandazi. Baada ya hapo weka donge lako pembeni na funika. Acha likae kwa muda wa nusu saa hadi saa moja.
3. Baada ya hapo chukua karai la mafuta weka jikoni acha hadi mafuta yapate moto kabisa.
4. Kisha chukua mashine ya kupikia tambi na weka donge lako. Kandamiza taratibu huku ukiruhusu minyororo ya tambi kuingia kwenye mafuta yaliyo jikoni.
5. Weka kiasi kiasi huku ukikaanga. Acha mpaka zitakapokuwa zimeiva na kukauka vizuri. Epua na weka pembeni. Weka kwenye sahani safi na kavu. Tambi zako zitakuwa tayari kwa kuliwa.



Mzee Rashid Msabaha - Sehemu ya II

KUJIUNGA NA JAMAAT.

Kujiunga kwake na Jumuiya kunanasibishwa na njozi aliyoota.

Alikuwa amekwenda katika msitu wa Jangwani (enzi hizo Jangwani ni pori kubwa) kwa ajili ya kutafuta Uwalii. (Daraja la kiroho katika Dini ya Islam).

Huko, alijitenga kwa siku kadhaa akifunga, kusali na kufanya maombi mbalimbali.

Siku moja akapata njozi. Katika njozi alijiona yuko pamoja na masheikh wake, yaani sheikh Idrisa na Sheikh Hashir. Mara kitu fulani chenye nuru kiliteremka kutoka mbinguni kikamfunika. Akawa anawafuata Masheikh wake huku akiwa amefunikwa na kile kitu chenye nuru. Ajabu kila akiwafuata, Masheikh wake wakawa wanamkimbia. (mwisho wa njozi)

Aliporudi kutoka jangwani akamhadithia sheikh Idrisa njozi yake. Sheikh hakujua taawili ya njozi ile. Akamshauri atafute kitabu cha tafsiri za ndoto kiitwacho Ta'atirul Anaam. Humo hakupata tafsiri ya njozi yake. Sheikh akamwambia tena atafute kitabu kingine kinaitwa Maashallah. Humo pia tafsiri haikupatikana. Basi njozi ikaendelea kumsumbua huku akiuliza hapa na pale nini maana yake.

Siku moja akakutana na Sheikh Kaluta Amri Abedi akiwa anahubiri kariakoo, akamuhadithia na kisha akamuuliiza iwapo anafahamu tafsiri ya njozi yake.

Sheikh Amri Abedi akamwambia afuatane nae hadi msikitini kwa sheikh Mubarak Ahmad. Sheikh Mubaraka akamtafsiria njozi yake kuwa, utapokea nuru ambayo ni ujumbe wa Allah.

Nuru yenyewe ni Mtume wa Allah aliyedhihiri zama hizi naye ni Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] ambaye ndiye mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya. Sheikh Mubarak akachukua kitabu kilichokuwa imeandika Hotuba maarufu ya Hadhrat Ahmad a.s 'khutba Ilhaamiyya' akamsomea maneno yasemayo "*wa anaa dhaalika Nuur..*". yakielezea kuwa, Hadhrat Ahmad ndio hiyo Nuru …".

Taawili aliyopewa na maneno hayo yakamuathiri roho na moyo wake, hakuwa na budi isipokuwa kumkubali mjumbe wa Allah na kujiunga na Jamaat.

Alipelekea habari kwa Masheikh wake juu ya taawili ya njozi yake na kumfahamisha kuwa amemtambua Imam wa zama na amejiunga na Jumuiya ya Ahmadiyya.

Sheikh Idrisa akamwambia wewe umeisha tanassar yaani umetoka nje ya Islam.

Akawaendea wanafunzi wenzake kuwapa habari hiyo, nao wakamkimbia!.

Njozi ikatimia barabbara.

Itaendelea Inshallah

Kifo Juu ya msalaba? Hoja kumi kutoka kwenye Biblia Takatifu

Kutoka toleo lililopita

4. MIKAKATI YA PILATO KUMUOKOA KRISTO.

Pilato, Gavana alikuwa na imani thabiti kuwa Yesu Kristo hakuwa na hatia, hivyo tangu awali alitengeneza mikakati ya kumuokoa. Kama afisa anayewajibika kwa himaya ya Roma asingeweza kuonesha Dhahiri mikakati yake ya kumsaidia Yesu Kristo, lakini yeye ndiye alikuwa uti wa mgongo wa mipango hiyo. Wahusika wengine katika mikakati hiyo ni pamoja na Yusufu wa Arimathea, diwani mwenye heshima na mfuasi wa Yesu Kristo. Mhusika mwingine katika mikakati hiyo alikuwa msomi Mmoja Nikodemasi ambaye alifahamu fika mikakti yote. Tunasoma katika Yohana: Akaenda Nikodemas naye, yule aliyemwendea usiku hapo kwanza akaleta mchanganyiko wa manemane na udi yapata ratili mia).

Pilato alifanya jambo la busara sana la kuchagua Ijumaa alasiri kuwa siku ya kumweka Yesu msalabani ili asiendelee kuwa msalabani jua likichwa, siku iliyokuwa inafuata ilikuwa Sabato, siku takatifu ya Wayahudi. Aliwachagua Yusufu na Nikodemasi marafiki wa karibu wa Yesu Kristo kukamilisha makakati huu uliokuwa tayari umekwisha pangwa. Hatua zote za kumfanya Yesu apate fahamu tena zilichukuliwa. Kama si hivyo Nikodemas alikuwa na maana gani kuleta mchanganyiko wa manemane na udi. Katika kumbukumbu za Serikali Yesu alielezwa kuwa amekufa ili kuwatuliza Wayahudi na Serikali ya huko Roma. Kwa ushujaa mkubwa Yusufu wa Arimathaya aliomba mwili wa Yesu kutoka kwa Gavana na bila kusita akapewa. Kama mkakati huu haukuwa umepangwa, Gavana angempaje mwili wa Yesu mtu ambaye si mweneyeji asiyejulikana? Kuna sababu ya kuamini kuwa hata Yesu Kristo naye aliufahamu mkakati huu ili bishara ile itimie kwani kama Yona alivyokuwa katika tumbo la samaki siku tatu mchana na usiku hivyo hivyo mwana wa Adamu atakuwa katika moyo wa nchi siku tatu mchana na usiku. Kukutana kwa Nikodemasi na Yesu Kristo usiku uliopita kunaweza kueleza kutokana na nadharia hii.

Itaendelea toleo lijalo

MATUKIO KATIKA PICHA







Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Zanzibar, Tanzania
Kambi hiyo ilipata mwakilishi wa Sadr Majlis ambaye ni Naib Sadr Tabligh, Mwl Suleiman Mubarak sahib.
Allah Awazidishie elimu ya Kidini Amin

Tarbiyyati Class Zanzibar, Tanzania
Tanzim ya Majlis Khudam-ul-Ahmadiyya Tanzania ilipanga kambi ya malezi kwa ajili ya Vijana wa











Wanafunzi na waalimu wa Jamia Ahmadiyya Tanzania katika Mkutano wa Sirat-un-Nabi[saw]
Allah Atujalie uwezo kufuata Mfano Mwema wa Mtume wetu mpendwa Muhammad[saw] Amin







Kambi ya Malezi ya Vijana wa Ugweno, Tanga.
Khuddam 17 na Atfal 9 walishiriki. Siku ya ufungaji waliongezeka Nasrat 17 na Ansarullah 4







Kambi ya Malezi ya Vijana wa Wilaya Ushetu, Shinyanga
Khuddam-ul-Ahmadiyya 103 kutoka matawi 21 ya wilaya Ushetu, Shinyanga walishiriki katika kambi ya malezi ya siku moja. Allah Awabariki sana, Amin

Umuhimu, Ubora na Fadhila za kumsalia Mtume saw



Na **Sheikh Karimuddin Shams**
Mbeya, Tanzania

Kutoka toleo Lililopita

Kupata utakaso na mafanikio

عن ابی ہریرۃ رضی اللہ عنہ قال قال رسول اللہ ﷺ صلّوا علیّ فَاِنَّ صَلٰوتَکم عَلیّ زَکٰوۃ لّکم
جلا، الافہام)

Hazrat Abu Hurairah[ra] anasimulia kuwa mtume ﷺ alisema: nisalieni mimi kwani kunisalia mimi ni chanzo cha kujitakasa kwenu na kupata mafanikio.

Kwa yakini hadithi hii mtume s.a.w ni tafsiri halisi ya aya ile ya Kurani Tukufu inayosema hivi:

هُوَالَّذِيْ يُصَلِّي عَلَيْكُمْ وَ مَلٰٓئِكَتُهٗ لِيخرجَكم مِنَ الظّلماتِ اِلى النّورِ ۔ (الاحزاب : ۴۴)

Yaani *Yeye ndiye Anayewarehemuni na Malaika Wake ili kuwatoeni kutoka giza na kuwapelekeni kwenye nuru.*

Kuna ufufunuo wa Hadhrat Ahmad[as] unaofichua siri hii kuwa;

وصلّ علی محمد و آلِ محمد اَلصّلاۃ ھوالمرتّی۔

Na msalieni Muhammad ﷺ na Aali zake Muhammad ﷺ kwani sala hiyo ndiyo itakayowaleeni, yaani sala ya Mtume ﷺ ni sababu ya malezi yetu ya kikhulka, kitabia na kiroho.

Safari moja Seyyedna Ahmad[as] alimuandikia bwana Rustam Ally sahib (sahaba wa Hazrat Ahmad as) akimjibu barua yake kwamba: soma sala hiyo tunayoisoma ndani ya sala (ya kila siku), kama inasomwa daima kwa uaminifu wa moyo na mapenzi halisi basi itakuwa pia sababu ya kumuona (mtume ﷺ kwenye ndoto au njozi n.k.) kisha inaleta athari nzuri juu ya kuangaza undani (mwa mtu husika) na kumuimarisha katika dini. (Maktubat-e-Ahmadiyya j.5.uk.7)

Dua hugota kati ya mbingu na ardhi

Imesimuliwa na Hazrat Omar bin Khattab ra kwamba: dua hugota kati ya mbingu na ardhi na maadamu humsalii Mtume saw, sehemu yoyote ya dua hiyo inakuwa haiendi juu (kupelekwa kwa Mwenyezi Mungu). (Tirmizi Abawabul Witri).

Kisha *imesimuliwa na Hazrat Fudhalah bin Ubaid[ra] kwamba Mjumbe wa Allah[saw] alimsikia mtu mmoja akiomba dua katika sala yake. Mtu huyu hakumtukuza Allah wala hakumsalia Mtume[saw]. Hapo Mtume[saw] alisema: huyu amefanya haraka. Kisha akamwita na kumwambia yeye ama mwingine kwamba: mmoja wenu anapoomba dua inampasa aanzie na kumhimidia Mola wake na kumsifu kisha amsalie Nabii[saw]. Kishapo aombe baadaye apendavyo.* (Abu Dawood kitabus Salat Bab-ud- dua)

Kupata msamaha wa madhambi

Hazrat Abu Bakri[ra] anasimulia kuwa kumsali Mtume[saw] kinafuta madhambi zaidi kuliko maji baridi jinsi yafutayo kiu na kumwombea Mtume[saw] amani kina ubora mkubwa zaidi hata kuliko kuwapa uhuru watumwa kisha kumpenda yeye ni jambo lenye fadhila zaidi kuliko kupigana jihadi au kuliko kuuawa katika njia ya Mwenyezi Mungu. (Tafsir Durre Mansoor)

Njia ya kuenda Peponi

Imesimuliwa na Hazrat Abdullah bin Abbas[ra] kwamba Mtume ﷺ alisema; anayeacha kunisalia mimi basi anaacha njia ya kuenda Peponi. (Sunan Ibne Majah)

Kisha kuna riwaya inayosema hivi kwamba, *mwenye kumsalia sana mtume ﷺ anaweza kushuhudia mahali pake huko Peponi akiwa hapo duniani.* (Jilaul Ifham)

Kupata ukaribu na Mtume ﷺ

Hazrat Abdullah bin Masood[ra] anasimulia kuwa, Mtume[saw] alisema: *"siku ya Qyama atakayekuwa karibu zaidi nami miongoni mwa watu ni yule atakayekuwa amenisalia zaidi miongoni mwao."* (Tirmizi Abawabul Witri…)

Kupata maombezi ya Mtume ﷺ

Hazrat Abu Bakr[ra] anasimulia kuwa; Mtume ﷺ alisema kwamba, atakayedumu kunisalia mimi basi mtu huyu atapata maombezi yangu siku ya Kiyama. (Jila ul Ifham)

Uzoefu wa dhati wa imamu wa Zama:

Hazrat Masihe Maud[as] anaeleza uzoefu wake binafsi wa kupata baraka za kumsalia Mtume[saw] akisema: *ilitokea hivi wakati fulani kwamba, nilishugulikia sana kumsalia Mtume[saw] kwa siku nyingi sana kwa kuwa nilikuwa na yakini kwamba njia za Mwenyezi Mungu ni nyembamba sana, bila ya kumpitia Mtume[saw] haziwezi kupatikana, kama vile hata Mwenyezi Mungu Anasema:*

وَابْتَغُوْٓا اِلَيْهِ الْوَسِيْلَةَ

(na mtafute njia kwake. Al-Maida 5:36)

Basi baada ya muda Fulani nikaona katika hali ya kashfi kwamba wachukuzi wawili wa maji wamekuja, mmoja akaingia nyumbani mwangu kwa mlango wa ndani na mwingine kwa mlango wa nje, walikuwa wamebeba mabegani mwao viroba vya nuru (na kuirusha ndani) na wakasema:

هٰذَا بِمَا صَلَّيْتَ عَلٰي مُحَمَّدٍ

Yaani baraka hizi ni kwa sababu ya wewe kumsalia Muhammad saw. (R.Kh.J.22.Uk.131 maelezo ya chini)

Kuondoa umaskini

Hazrat Jabir bin Samura[ra] anasimulia kwamba, Mtume ﷺ alisema: kumkumbuka Mwenyezi Mungu kwa wingi na kunisalia mimi ndio chanzo cha kuondoa umaskini. (Jila ul Ifham)

Sala ya Mtume ﷺ ipi bora zaidi

Hazrat Ahmad[as] aliyetumwa na Mwenyezi Mungu kuwa Hakimu Mwadilifu wa zama hizi anasema kwamba sala ya Mtume ﷺ iliyo bora kabisa ni ile tu aliyoifundisha Mtume ﷺ mwenyewe nayo ni kama ifuatayo:

اَللّٰھمَّ صَلِّ علي محمد و علي آل محمد کما صلیت علي ابراھِیم وعلي آل ابراھِیم انک حمید مجید. اللھم بارك علي محمد و علي آل محمد کما بارکت علي ابراھیم و علي آل ابراھیم انك حمید مجید.

Kisha seyyidna Ahmad[as] anasema: *sala ya Mtume ﷺ yenye mibaraka zaidi ndio ile tu iliyofundishwa na Mtume ﷺ nami pia naisoma hiyo.*

Wakati wa kuisoma sala ya Mtume ﷺ

Sala ya mtume ﷺ ni dua inayojijumuisha maombi ya kila namna ndani yake na kuondoa shida, taabu na matatizo ya namna zote. Kwa kweli hatuna haja ya kuomba dua yoyote baada ya kuomba dua hii na dua hii pia inaweza kuombwa muda wowote kama dua yoyote nyingine, tunaweza kumsalia Mtume ﷺ wakati wowote, asubuhi, mchana, jioni na kabala ya kulala wakati wa usiku mara baada ya kuamka, ndani ya sala ya Tahajjudi au ndani ya sala zetu za kawaida n.k. na kama mtu yeyote anapenda kuisoma kwa kupanga muda fulani basi maandiko yafuatayo ya Hadhrat Ahmad[as] yatampa mwongozo, yeye anasema kuwa; ***tuisome sala ya Mtume ﷺ kwa wingi baada ya sala ya Magharibi na Ishaa jinsi tuwezavyo na kuisoma kwa uaminifu na mapenzi ya moyo na kama inapangwa kuisoma mara 1100 au 700 kwa siku basi itakuwa bora zaidi.***

Kupanga idadi maalum kwa ajili ya kuisoma sala ya Mtume saw kwa siku:

Watu wengi wanaweza kuuliza kuwa tuisome mara ngapi ndani ya siku moja?

Seyyedna Ahmad[as] anasema akijibu swali la namna hii kuwa; *si lazima kupanga idadi Fulani tu, inatakiwa kuisoma (sala ya Mtume ﷺ) kwa ikhlasi, uaminifu, uyenyekevu na kwa moyo mkunjufu na kuendelea kuisoma hadi pale inapopatikana hali ya kujipoteza na kuzama kwenye huba ya Mtume ﷺ na kupata hali ya kuipanuka kwa moyo n.k.* (Maktubat e Ahmadiyya j.1.uk.18)

Ikumbukwe kuwa, kuna baadhi ya riwaya zinaeleza idadi maalum ya kuisoma sala ya mtume ﷺ na Hazrat Masihe Maud[as] pia aliwaambia baadhi ya maswahaba zake kwa ajili ya kuisoma hadi mara 1100 kwa siku ila nadhini hiyo ni sawa na hali zao za dhati na mtu yeyote anaweza kupanga idadi maalum kutokana na tabia yake halafu muradi wa mara 100, 200, 300, 700 au 1100 kwa siku pia inaweza kuwa kuisoma kwa wingi.

Hazrat Aqdas Masihe Maud[as] anasema: *"kwa sababu ya sala ya Mtume ﷺ …naona baraka za Mwenyezi Mungu zinaelekea kwa Mtume ﷺ kwa sura ya ajabu ya nuru na halafu bada ya kufika huko zinapenya ndani ya kifua cha Mtume ﷺ na baada ya kutoka humo zinageuka kuwa mifereji mingi isiyohesabika na zinamfikia kila anayestahili kuzipata kwa kiwango chake. Kwa yakini hakuna baraka iwezayo kufika kwa watu wengine bila ya kupitia kwa Mtume ﷺ. Sala ya Mtume ni nini? Ni kuitikisa arshi ile ya Mtume ﷺ ambamo yabubujika hiyo mifereji ya nuru. Yule anayetaka kupata baraka na Fadhila za Mwenyezi Mungu yamlazimu amsalie sana Mtume ﷺ ili baraka hiyo ipate kutikisika.* (Al-Hakam, 28 Feb.1903.uk.7)

Hivyo basi sisi sote tunatakiwa kumsalia sana bwana wetu mpendwa Mtume ﷺ ili tupate rehema, baraka na heri nyingi za kila namna.

Khalifa wetu wa Tano Hazrat Mirza Masroor Ahmad ATBA anasema: *"Mwenyezi Mungu amewasisitizia sana waaminio kuhusu kumsalia Mtume saw kuna nini sababu yake? Je Mtume saw anahitaji maombi yetu? Hapana (Yeye hahitaji kabisa). Bali tumefundishwa njia hii kuwa: Enyi watumishi wangu! Mnaponiletea haja zenu, mnapofika kwangu, ili maombi yenu yapokelewe na kutimizwa kwa haja zenu, basi mna (weza kutumia) njia moja tu nayo ni hii kwamba mufike kwangu kupitia Mtume wangu saw. Kama hamtatumia njia hii basi ibada zenu zote zitapotea bure kwani vitu hivi vyote, ulimwengu huu wote nimeviumba kwa ajili ya Mtume huyu mpendwa wangu ﷺ* (Khutbate Masroor J.1.UK.288)

Kama imeelezwa katika hadithi kuwa: Mwenyezi Mungu Anasema: *"kama nisingekuumba wewe basi nisingeumba ulimwengu huu"* (Mauzuate Kabiir uk.325)

Ningependa kuimalizia kwa dua ifuatayo ya Hazart Ahmad[as] kwa ajili ya bwana wake Mtukufu Mtume Muhammad ﷺ Kwamba:

اللھم صَلِّ و سَلِّم وبَارِک عَلیہِ و آلِہِ بِعَدَدِ ھَمِّہ و غَمِّہ و حزنہ لِھذِہِ الامّۃِ و انزِل علیہ انوار رحمتک الی الابد ۔

Tafsiri; *E, Allah umsalie Mtume saw na Wafuasi wake na kumshushie rehema baraka na salamu zako kwa kadiri alivyokuwa na hanu, huzuni na kuhangaika kwa ajili ya umma kisha Uendelee kumteremshia nuru ya rehema na baraka zako daima dwamu. Aamin.* (Baraka za Dua, Rohani Khazain J.6.uk.11)

Makhalifa Walioongoka - Hadhrat Abu Bakar ra

Kutoka uk. 12

kuhusu kuondoka kwa Mtukufu Mtume ﷺ kutoka Makka, na walikuwa wakingojea kuwasili kwake. Siku moja, Myahudi mmoja akiwa amesimama juu ya kilima alimwona Mtukufu Mtume ﷺ na Hadhrat Abu Bakr ra wakikaribia na akawatangazia Waislamu kwamba kiongozi wao amewasili. Waislamu wakatoka mbio kwenda kuwapokea. Walipowafikia, Hadhrat Abu Bakr ra alisimama, huku Mtukufu Mtume ﷺ akiwa amekaa kimya. Baadhi ya watu wa Madina ambao walikuwa bado hawajamuona Mtukufu Mtume ﷺ kwanza walimwendea Hadhrat Abu Bakr ra na wakaanza kumsalimia wakimdhani kuwa yeye ndiye Mtukufu Mtume ﷺ. Wakati huo, Hadhrat Abu Bakr ra akalichukua joho lake na kumkinga Mtume Mtukufu ﷺ na jua, ambapo kwa njia hiyo watu walitambua kwamba yupi alikuwa ndiye Mtukufu Mtume ﷺ.

Msingi Wa Msikiti Wa Quba Ukawekwa, Na Sala Ya Kwanza Ya Ijumaa Ikasalishwa

Hadhrat Khalifatul Masih V atba alisema kuwa imeandikwa kwamba Mtukufu Mtume ﷺ alikaa Quba kwa muda wa siku kumi. Wakati wa kukaa huku, Mtukufu Mtume ﷺ aliweka msingi wa msikiti, unaojulikana kama Msikiti wa Quba. Mtukufu Mtume ﷺ alisema kwamba msingi wa msikiti huu uliwekwa juu ya uchamungu.

Hadhrat Khalifatul Masih V atba alisema kuwa baada ya kukaa Quba, Mtume Mtukufu ﷺ akaondoka kuelekea Madinah. Akiwa njiani, Mtume Mtukufu ﷺ alipokuwa kwenye bonde la Banu Salim bin Auf, ukawadia wakati wa Sala ya Ijumaa. Hivyo, Mtume Mtukufu ﷺ akasali Sala ya Ijumaa katika Msikiti wa bonde la Ranunah pamoja na Waislamu 100. Msikiti huo ukaanza kujulikana kwa jina la Msikiti wa Sala ya Ijumaa, kwa vile hii ilikuwa Sala ya kwanza ya Ijumaa aliyoisalisha Mtume Mtukufu ﷺ katika Madinah.

Hadhrat Khalifatul Masih wa Tano atba alifafanua kuwa huo Msikiti huenda ukajengwa rasmi baadaye.

Hadhrat Khalifatul Masih wa Tano atba alisema kuwa baada ya kusali Ijumaa, Mtume Mtukufu ﷺ akaendelea na safari yake ya kuelekea Madinah, kwa kupanda ngamia wake pamoja na Hadhrat Abu Bakr ra akiwa nyuma yake.

Furaha Kwa Ufikaji Wa Mtume Mtukufu ﷺ Katika Madinah

Hadhrat Khalifatul Masih wa Tano atba alisema kuwa Buraidah alikuwa mtu mwingine aliyeshawishika na zawadi ya kumkamata Mtume Mtukufu ﷺ, iliyotangazwa na wakazi wa Makkah. Hivyo yeye akaondoka na watu sabini kutoka kabila la Banu Sahm. Wao walipomfikia Mtume Mtukufu ﷺ akamwuliza kuwa yeye ni nani, na ametoka wapi, na Buraidah akamweleza. Na Buraidah alipomwuliza kuwa yeye ni nani, Mtume Mtukufu ﷺ akamjibu kuwa, yeye ni Muhammad mwana wa Abdullah, Mtume wa Allah. Hapo Buraidah akajiunga na Uislamu pamoja na wale wote waliokuwa naye. Keshoye, yeye akasema kuwa Mtume Mtukufu ﷺ anatakiwa kuingia Madinah pamoja na bendera. Hivyo akatoa kilemba chake, na kukifunga juu ya mkuki wake na akawa anatembea mbele ya Mtume Mtukufu ﷺ alipokuwa anaingia Madinah.

Hadhrat Khalifatul Masih wa Tano atba alisema kuwa, Mtume Mtukufu ﷺ aliendelea na msafara wake pamoja na Waislamu kuelekea mji wa Madinah. Yeye alipokuwa anapita karibu na nyumba za watu, wao wakawa wanamwomba kwamba yeye aishi katika nyumba zao, na Mtume ﷺ akawa anawaombea dua. Wanawake na watoto wakasimama kwenye paa za nyumba zao wakiimba nyimbo za kumkaribisha Mtume Mtukufu ﷺ. Mtume Mtukufu ﷺ akawafikia watu wa Banu Najjar waliokuwa wamesimama kwa mpangilio wakivaa silaha zao kwa kumkaribisha Mtume Mtukufu ﷺ. Na wanawake wa Banu Najjar walikuwa wanaimba nyimbo za shukrani na kumsifu Mtume Mtukufu ﷺ.

Hadhrat Khalifatul Masih V atba alisema kuwa, baada ya siku chache Mtume Mtukufu ﷺ akamtuma Hadhrat Zaid bin Haritha ra kuelekea Makkah, ili awalete Madina jamaa zake na vitu vilivyosalia kule. Mtume Mtukufu ﷺ akanunua uwanja fulani katika Madina, ambapo kwanza akauweka msingi wa Msikiti, na kisha akaanza kujenga nyumba kwa ajili yake na kwa ajili ya Masahaba wake ra. Hadhrat Abu Bakr ra akakaa katika mahali palipokuwa karibu na Sun'a, na palikuwa umbali wa maili mbili kutoka mjini Madinah.

Hadhrat Khalifatul Masih V atba alisema kuwa, ataendelea kuangazia matukio ya maisha ya Hadhrat Abu Bakr ra katika hotuba zijazo.

Sala ya Jeneza:

Hadhrat Khalifatul Masih wa Tano atba alisema kuwa ataongoza Sala ya jeneza ya ghaib kwa baadhi ya Wanajumuiya waliofariki dunia hivi karibuni.

Bw. Chaudhari Asghar Ali Kilaar:

Bw. Chaudhari Asghar Ali Kilaar aliyekuwa mahabusu katika njia ya Mwenyezi Mungu. Alifariki tarehe 10 Januari akiwa gerezani. Hadhrat Khalifatul Masih wa Tano atba alisema kuwa kwa hivyo atahesabiwa kuwa shahidi katika njia ya Mwenyezi Mungu. Alikamatwa tarehe 24 Septemba, 2021 katika Bahawalpur, Pakistan baada ya kushtakiwa chini ya sheria za Pakistan za kukufuru. Afya yake ikaharibika akiwa gerezani, kwa sababu hiyo akapelekwa hospitalini tarehe 4, alipofariki baadaye katika umri wa miaka 70, baada ya kuwa kizuizini kwa muda wa miezi mitatu na siku 15.

Hadhrat Khalifatul Masih wa Tano atba alitukumbusha kuwakumbuka mahabusu wote katika njia ya Mwenyezi Mungu ndani ya maombi yetu.

Bw. Mirza Mumtaz Ahmad

Bw. Mirza Mumtaz Ahmad mfanyakazi wa ofisi ya Wakalat Ulya, Rabwah. Aliitumikia Jumuiya muda mrefu mno. Ameacha nyuma yake mke wake, wana wawili na binti mmoja. Alikuwa na sifa nyingi nzuri na alikuwa amejitolea sana katika kazi yake.

Col. Dr. Abul Khaiq:

Col. Dr. Abdul Khaliq msimamizi mstaafu wa Hospitali ya Fazle Umar, Rabwah. Ameacha nyuma wana wawili na binti wawili. Wakati Pakistani ilipotangaza Waislamu Waahmadiyya kuwa sio Waislamu, yeye akajiuzulu kutoka kazi hiyo ya serikali. Na akajitolea muhanga kuitumikia Jumuiya chini ya ofisi ya Nusrat Jahan Scheme. Yeye akatumwa Siera Leon, ambapo akahudumu kwa miaka mitatu. Akahudumu katika Samarkand pia, kule akawasaidia watu wengi na pia akaubashiri ujumbe wa Jumuiya.

Hadhrat Khalifatul Masih V atba aliomba kuwa, Mwenyezi Mungu Awatendee wote kwa msamaha na huruma na Awajaalie watoto wao uwezo wa kuendeleza mema yao.

Uchawi - Imani za kishirikina

Kutoka uk.11

hivyo waka muweka Nabii kwenye daraja kama lao wakidhani kuwa kawashinda katika elimu au utaalam wa mazingaombwe yao. Kumbe wo wameshindwa kujua upi uongo na upi ukweli kulingana na jamii yao walio kuwa wanaishi walizungukwa na watu wasio mtambua Mungu na wamejikita kwenye udanganyifu kwa kupata manufaa ya kidunia tu.

2 Huu ndiyo mtazamo tunao ishi nao leo katika karne ya 15 tangu Quran ilipo teremshwa , kwani waislam wengi wamejikita katika kutafuta maisha ya dunia kwa njia yeyote ile na hasa udanganyifu kwa kutumia aya za Quran vibaya na Hadithi za Mtume [s.a.w] kama sehemu ya kujifichia kwa wale wasio jua dini ili wapate kuwadanganya na kufanya wanacho taka. Hivyo unakuta watu wana acha kumwamini Allah kisawasawa wana amini maombi ya sheikhe tu yanatosha.

HADITHI ZA Mtume [S.A.W] JUU YA SHIRKI

Imesimuliwa na Ibn Mas'oud [r.a] ya kwamba Mtume s.a.w alisema hirizi ni shirk,hirizi ni shirki, hirizi ni shirki maneno haya aliyatamka mara tatu.[Abuu dawuud kitaab tibbi baab tayyarah].

Sasa katika jamii tunazo ishi sasa jambo hili limekuwa la kawaida na watu wana imani nalo sana kwamba hirizi inaweza mkinga mtu na balaa Fulani na hasa watoto wana vishwa ili waweze kulindwa na watu wenye uchawi kama inavyo sadikika, ilhali kitu hicho ni imani potofu na kina mpeleka mtu mbali na Mungu wake. Imani hii imepandikizwa vichwani mwa watu toka karne nyingi zilizo pita kiasi kwamba kwasasa ukimwambia mtu hivyo vitu havisaidii kitu na wala havina maana, basi mtabishana na mtu huyo na hato kubali. Kitendo cha kumvisha mtoto hirizi ndiyo anafundishwa toka utotoni kuwa uchawi upo na anahitaji kujikinga, madhara ya vitendo hivi ni haya kuwa endapo wazazi watazeeka na watoto wao wakapata watoto wale wajukuu wata anza kuwaita bibi au babu mchawi na mwisho wa siku nao wanaenda kwa waganga wa kienyeji kuagua kisha hao waganga wana waambia kuwa bibi yako huyo au babu yako huyo na muda mwingine siyo mjukuu ni mtoto wako wa kumzaa anakuja kukuita wewe mchawi na kupanga njama za kukuuwa.

Imesimuliwa na Hadhrat Abuhuraira [r.a] ya kwamba Mtume [s.a.w] amesema, hirizi haina maana, hirizi nzuri ndiyo nzuri, akaulizwa hirizi hiyo nzuri ni nini? Akajibu maneno mazuri ambayo mmoja wenu anasikia.

Hapa Mtume saw kaweka wazi kuwa hirizi haina maana ila hirizi nzuri ni maneno mazuri ambayo mmoja wenu huyasikia. Sasa tujiulize kulogana ni maneno mazuri au kuna faida gani na familia ipi iliyo endelea wakawa pamoja kwa kufanya mambo haya?

Niwajuze kitu nduguzanguni katika imani kwamba katika ulimwengu wa leo ulio endelea hao wanaoitwa waganga wanacho fanya ni upelelezi kwanza kujua jamii Fulani au mtu Fulani ana amini maswala ya uchawi? Na kama wakijuwa ni kweli basi Yule aliye kuja kufanya upelelezi anaenda toa taarifa kwa mganga wake sasa siku utakuja kuona mtu ana kwambia mambo mbayo akili yako inakubali na hapo ndiyo mwanzo wako wa kukubali kila anacho kwambia na kukutaka utoe pesa nyingi na hata kufanya vitu vya kuhatarisha uhai wa mtu ili akupe dawa ya kujikinga na wewe utakubali.

Ukiangalia zile familia zinazo ishi katika hali hii asilimia tisini hazielewani na mpasuko ni mkubwa na unakuta Yule aliye na uwezo hawezi saidia nduguze na nduguze wata anza mwita mchawi ndiyo maana mali yake hataki kusaidia wengine.

Sasa tujue ya kwamba haya ni mambo ya kusikitisha na hayapo katika mafundisho ya Islam.

Amesema mjumbe wa Allah s.a.w] ya kwamba; *yeyote anae mwendea mwaguzi wa nyota sala yake haita*

Itaendelea toleo Lijalo

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

Mapenziya Mungu

JAM. II - RAJAB. 1443 AH | FEBRUARI 2022 | TABLIGH 1401 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu^{saw}

Imesimuliwa na Hadhrat Ibn Mas'ud r.a. ya kwamba Mjumbe wa Allah^{saw} alisema: Mkiwa watatu, basi wawili kati yenu wasinong'onezane kwa kumwacha yule wa tatu mpaka mchanganyike na watu, kwani jambo hilo litamhuzunisha huyo (**Muslim**).

Makhalifa Walioongoka - Hadhrat Abu Bakar^{ra}

Katika hotuba ya Ijumaa iliyotolewa Masjid Mubarak tarehe 04/01/2022; Baada ya Tashahhud, Ta'awwudh na Surat Faatihah, Khalifa Mtukufu V, Hazrat Amir ul Momeniin, Mirza Masroor Ahmad^{atba} ('Ayyadahullahu Ta'ala Bi-Nasrihil Aziiz') alisema kwamba ataendelea kuangazia matukio kutoka maisha ya Hadhrat Abu Bakar^{ra}.

Suraqah bin Malik Anamfuata Mtukufu Mtume^{saw}

Hadhrat Khalifatul Masih V^{atba} alisema kuwa watu wa Makka walikuwa wametangaza zawadi kwa mtu yeyote ambaye angeweza kuwakamata Mtume^{saw} na Hadhrat Abu Bakr^{ra}. Hivyo, watu kama vile Suraqah walijaribu kumtafuta Mtukufu Mtume^{saw} wakati yeye na Hadhrat Abu Bakr^{ra} walipokuwa wakihama. Hata hivyo, Mwenyezi Mungu Hakumwezesha kufanikiwa kuwakamata.

Hivyo, alimwomba Mtukufu Mtume^{saw} ulinzi siku atakapoingia Makkah akiwa mshindi. Mtukufu Mtume^{saw} kisha akambashiria Suraqah kwamba siku moja atavaa bangili za Khusro (Mfalme Mkuu Wa falme za Kiirani). Baadaye, katika zama za Hazrat Umar^{ra}, wakati Khusro alipoangushwa, Hazrat Umar^{ra} alimuita Suraqah na kumpa bangili za Khusro, na hivyo kutimiza utabiri uliotolewa na Mtukufu Mtume^{saw}.

Hadhrat Khalifatul Masih V$^{(atba)}$ alisema kuwa Suraqah alipokuwa anarudi baada ya kukutana na Mtume Mtukufu^{saw}, yeye akakutana na msafara mwingine wa wakazi wa Makkah, uliokuwa umeondoka pia kwa lengo la kumtafuta Mtume Mtukufu^{saw}. Wakati Suraqah alipozungumza nao, hakutaja chochote kuhusu mahali alipo Mtukufu Mtume^{saw}. Kwa hakika, alizungumza nao kwa namna hii kwamba, hata wakashawishika kusitisha utafutaji wao na wakurudi.



Masjid Mubarak: Hadhrat Khalifatul Masih V^{atba} huhutubia Ijumaa kwa waaminio tokea na kurushwa duniani kote kwa njia ya satelaiti.

Tukio Moja la Bi Ummi Ma'bad

Hadhrat Khalifatul Masih V$^{(atba)}$ alisema kwamba wakati wakiwa safarini, Mtukufu Mtume^{saw} na Hadhrat Abu Bakr^{ra} walipita kwenye boma la mwanamke mmoja aitwaye Ummi Ma'bad, na wakauliza kama alikuwa na chakula chochote, nyama au tende ambayo wao wangeweza kununua kutoka kwake, hata hivyo hakuwa na chochote kwani watu wake walikuwa wakipitia nyakati za shida na njaa kipindi hicho. Mtukufu Mtume^{saw} alimuona mbuzi kwenye pembe moja ya boma na akamuuliza kuhusu huyo. Ummi Ma'bad alisema kwamba mbuzi huyo alikuwa dhaifu sana, kiasi kwamba hakuweza hata kwenda malishoni na hakuweza kutoa maziwa. Mtukufu Mtume^{saw} aliomba idhini kama angeweza kujaribu kumkamua. Hivyo, Mtukufu Mtume^{saw} akaomba dua, na kisha akamkamua, mbuzi huyo akatoa maziwa mengi, mengi kiasi hiki kwamba kundi zima la watu likaweza kunywa maziwa yake. Mtukufu Mtume^{saw} alimpa Ummi Ma'bad maziwa na yeye akanywa akashiba, na baada ya hapo Mtukufu Mtume^{saw} mwenyewe akanywa baadhi. Kisha akaacha ndoo moja ya maziwa kwa Umm Ma'bad, akamnunua yule mbuzi na akaendelea na safari yake.

Hadhrat Khalifatul Masih V^{atba} alisema kuwa wapinzani wa Mtume Mtukufu^{saw} katika mahangaiko ya kumtafuta kwao yeyena Hadhrat Abu Bakar^{ra} walifika pale na kumwuliza Ummi Ma'bad kuhusiana nao. Mama huyo akakataa kuwaambia chochote, na wao walipoonyesha hasira na wakawa wakali, Ummi Ma'bad akawajibu kwa ushujaa kuwa wao wasipoondoka hapo, atawaita watu wa kabila lake watakaowashambulia. Hivyo, wakazi wa Makkah wakaondoka.

Hadhrat Khalifatul Masih V^{atba} alisema kuwa njiani, Mtume^{saw} alikutana na Hazrat Zubair^{ra} ambaye alikuwa anarudi na msafara wa biashara kutoka Syria. Hadhrat Zubair^{ra} aliwapatia nguo nyeupe wote Mtukufu Mtume^{saw} na Hadhrat Abu Bakr^{ra}.

Hadhrat Khalifatul Masih V^{atba} alisema kwamba wakiwa katika safari yao, wakakutana na misafara mbalimbali ya wafanyabiashara ambao waliweza kumtambua Hadhrat Abu Bakr^{ra} kwa vile yeye alikuwa pia mfanyabiashara, hata hivyo hawakuweza kumtambua Mtukufu Mtume^{saw}. Wakati walipokuwa wakimuuliza Hadhrat Abu Bakr^{ra} kuwa huyo ni nani, yeye akawa anawajibu kuwa huyu ni kiongozi wangu mwenye kuniongoza njia.

Kuwasili Quba Wakati wa Kuhama

Hadhrat Khalifatul Masih V^{atba} alisema kwamba baada ya siku nane za safari, walifika Quba siku ya Jumatatu, ambayo ni maili mbili hadi tatu kutoka Madina. Watu wa Madina walikuwa wamesikia

Endelea uk 11



KITABU

Baadhi ya Hadithi za Mtume^{saw}

Kijitabu hiki kinawasilisha misemo mbalimbali ya Mtukufu Mtume Muhammad, rehema na amani iwe juu yake, iliyochaguliwa kati ya mikusanyo mingi inayopatikana katika juzuu kadhaa.

Uteuzi huu wa maneno unakusudiwa kuwapa wasomaji muhtasari wa jumla wa mwongozo uliotolewa na Mtukufu Mtume saw na kuwahanikiza kutafiti zaidi Hadith na maneno ya Mwanzilishi Mtukufu wa Islamu ili kuongeza elimu yao. Kijitabu hiki kidogo lakini muhimu kilichapishwa kwanza kwa Kiingereza. Tafsiri yake ya kwanza ya Kiswahili ilionekana mnamo 1988.

Jipatie nakala yako kwa bei ya maktaba karibu nawe!

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com